***HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI NA MADINI MHE. PROF. SOSPETER MWIJARUBI MUHONGO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2016/17***

**ORODHA YA VIFUPISHO**

| | | |
|---|---|---|
| AFD | - | French Agency for Development |
| AfDB | - | African Development Bank |
| AGG | - | Airborne Gravity Gradiometer |
| BADEA | - | Bank of Arab for Economic Development in Africa |
| BGR | | Federal Institute for Geosciences and Natural Resources |
| BPS | - | Bulk Procurement System |
| CAMARTEC | | Centre for Agriculture Mechanization and Rural Technology |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CIDA | - | Canadian International Development Agency |
| CIF | - | Climate Investment Fund |
| CNG | - | Compressed Natural Gas |
| CNOOC | - | China National Offshore Oil Company |
| EAPP | - | Eastern African Power Pool |
| EPP | - | Environmental Protection Plan |
| EU | - | European Union |
| EWURA | - | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| FEMATA | - | Federation of Miners Association of Tanzania |
| FTG | - | Full Tensor Gradiometry |
| GIZ | - | Deutsche Gesellschaft fur Internationale Zusammenarbeit |
| GST | - | Geological Survey of Tanzania |
| GWh | - | Gigawatt Hour |
| HFO | - | Heavy Fuel Oil |
| ICEIDA | - | Icelandic International Development Agency |
| JBIC | - | Japan Bank for International Cooperation |
| JICA | - | Japan International Corporation Agency |
| KfW | - | Kreditanstalt fur Wiederaufbau |
| KIA | - | Kilimanjaro International Airport |
| kV | - | Kilovolt |
| Kva | - | Kilovolt-Ampere |
| LNG | - | Liquefied Natural Gas |
| LPG | - | Liquefied Petroleum Gas |
| Mb. | - | Mbunge |
| MCC | - | Millenium Challenge Corporation |
| MDAs | - | Mining Development Agreements |
| Mhe. | - | Mheshimiwa |
| mmscfd | - | Million standard cubic feet per day |
| MoU | - | Memorandum of Understanding |
| MPPA | - | Model Power Purchase Agreement |
| MRI | - | Mineral Resource Institute |
| MW | - | Megawatt |
| NACTE | - | National Council for Technical Education |
| NDC | - | National Development Corporation |
| NORAD | - | Norwegian Agency for Development Cooperation |
| OC | - | Other Charges |
| OMCTP | - | Online Mining Cadastre Transactional Portal |
| ORIO | - | Facility for Infrastructure Development (The Netherlands) |
| PAET | - | Pan African Energy Tanzania Limited |
| PBPA | - | Petroleum Bulk Procurement Agency |

| | | |
|---|---|---|
| PE | - | Personal Emolument |
| PICL | - | Petroleum Importation Coordinator Limited |
| PURA | - | Petroleum Upstream Regulatory Authority |
| QDS | - | Quarter Degree Sheet |
| REA | - | Rural Energy Agency |
| REMAS | - | Regional Miners Associations |
| SAPP | - | Southern African Power Pool |
| SCADA | - | Supervisory Control And Data Acquisition |
| Sida | - | Swedish International Development Cooperation Agency |
| SMBC | - | Sumitomo Mitsui Banking Corporation |
| SMMRP | - | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| SREP | - | Scaling-Up Renewable Energy Program |
| SSMP | - | Sustainable Solar Market Packages |
| STAMICO | - | State Mining Corporation |
| TAMIDA | - | Tanzania Mineral Dealers Association |
| TANESCO | - | Tanzania Electric Supply Company Limited |
| TASPA | - | Tanzania Salt Producers Association |
| TAWOMA | - | Tanzania Women Miners Association |
| TAZAMA | - | Tanzania - Zambia Pipeline Limited |
| TCF | - | Trillion Cubic Feet |
| TCPCO | - | Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited |
| TEDAP | - | Tanzania Energy Development and Access Expansion Project |
| TEITI | - | Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative |
| TGC | - | Tanzania Gemological Centre |
| TGDC | - | Tanzania Geothermal Development Company Limited |
| TIB | - | Tanzania Investment Bank |
| TIPER | - | Tanzania International Petroleum Reserve |
| TMAA | - | Tanzania Minerals Audit Agency |
| TPC | - | Tanganyika Planting Company Sugar Estate Limited |
| TPDC | - | Tanzania Petroleum Development Corporation |
| TRA | - | Tanzania Revenue Authority |
| UA | - | Unit of Account |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | - | United Nations Development Programme |
| UNEP | - | United Nations Environment Programme |
| USAID | - | The United States Agency for International Development |
| USD | - | United States Dollar |
| VETA | - | Vocational Education Training Authority |
| VVU | - | Virusi vya UKIMWI |
| WB | - | World Bank |
| WDL | - | Williamson Diamonds Limited |
| ZTK | - | Zambia – Tanzania – Kenya |

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI NA MADINI MHE. PROF. SOSPETER MWIJARUBI MUHONGO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2016/17

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2015/16 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2016/17.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwasilisha Hotuba hii kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. Uchaguzi huo uliwezesha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM). **Nampongeza kwa ushindi huo uliodhihirisha kukubalika kwake kwa Watanzania, hususan kutokana na uchapakazi na ufuatiliaji wake wa masuala ya maendeleo**. Ni ukweli usiopingika kwamba maamuzi anayoyachukua na mbinu anazozitumia katika kuongoza Taifa letu ni za kipekee na zinatakiwa kuungwa mkono na kila Mtanzania bila kujali tofauti ya itikadi zetu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuandika historia mpya ya nchi yetu ya kuwa Mwanamke wa Kwanza kushika wadhifa huo. Hii ni ishara njema kwa nchi yetu katika kuongeza nafasi za juu za wanawake katika Uongozi wa Taifa letu.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, natumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nakupongeza wewe binafsi Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nimpongeze Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** natumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu kwa kuniteua kuongoza Wizara ya Nishati na Madini. Niwahakikishie Watanzania kwamba

nitatumia weledi na uzoefu wangu wote katika kuhakikisha kuwa Sekta za Nishati na Madini zinaleta manufaa makubwa ya kiuchumi kwa Taifa letu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mhe. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mhe. Deogratias Francis Ngalawa (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Vilevile, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao katika kuendeleza na kusimamia Sekta za Nishati na Madini. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuteuliwa kwao kuwawakilisha wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo yafuatayo ni maelezo ya Mapitio ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2015/16 pamoja na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2016/17.

## A. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2015/16 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17

9. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015/16, Wizara ya Nishati na Madini iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangwa. Katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara iliidhinishiwa na Bunge Jumla ya **Shilingi bilioni 642.12**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 502.30** sawa na **asilimia 78** ya Bajeti yote zilikuwa ni Bajeti ya Maendeleo. Aidha, **Shilingi 139.82**, sawa na **asilimia 22** ya Bajeti yote zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara na Taasisi zake.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo Bajeti hiyo iliongezeka kutoka **Shilingi bilioni 642.12** hadi **Shilingi bilioni 762.12.** Lengo la ongezeko ni kutekeleza miradi mikubwa ya kufua umeme ukiwemo Mradi wa Kinyerezi II - MW 240 ili kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2016, Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi bilioni 565.51.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 506.28** sawa na **asilimia 90** zilikuwa ni za Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa **Shilingi bilioni 472.93** sawa na **asilimia 93** ya fedha za Maendeleo zilizopokelewa na **Shilingi bilioni 33.35** sawa na **asilimia 7** ni fedha za nje. Kiasi kilichobaki cha **Shilingi**

**bilioni 59.23** sawa na **asilimia 10** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 215.98** sawa na **asilimia 75** ya lengo la **Shilingi bilioni 286.66**. Kasi ya makusanyo ya mapato imepungua kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa shughuli za utafiti na uzalishaji wa madini kutokana na kushuka kwa bei za madini kwenye Soko la Dunia.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 370.68** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 29** ikilinganishwa na lengo la Mwaka 2015/16. Ongezeko hilo litatokana na mauzo ya Gesi Asilia. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kuziba mianya ya utoroshaji madini, kuimarisha ukaguzi wa uzalishaji na usafirishaji madini pamoja na kuboresha mazingira ya Wachimbaji Wadogo wa madini. Vilevile, Serikali itaboresha mfumo wa masoko ya madini ndani ya nchi kwa ajili ya kuongeza ushindani wa bei ili kuongeza mapato ya Serikali.

**SEKTA YA NISHATI**

**SEKTA NDOGO YA UMEME**

(i) **Hali ya Uzalishaji Umeme**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini (*total installed capacity*) umeongezeka kutoka **MW 1,226.24** mwezi Aprili, 2015 hadi **MW 1,461.69** mwezi Aprili, 2016 sawa na ongezeko la **asilimia 19**. Ongezeko hilo limechangiwa na mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia baada ya kukamilika kwa Bomba la kusafirisha Gesi Asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam. Kati ya uwezo huo, MW 711.00 (**asilimia 49**) ni Gesi Asilia, MW 566.79 (**asilimia 39**) zinatokana na umeme wa nguvu za maji na MW 183.90 (**asilimia 12**) ni mafuta na tungamotaka. Aidha, mahitaji ya juu ya umeme yameongezeka kutoka **MW 988.27** mwezi Desemba, 2015 hadi kufikia **MW 1,026.02** mwezi Machi, 2016 sawa na ongezeko la **asilimia 4**.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kiasi cha umeme kilichoingizwa kwenye Gridi ya Taifa kiliongezeka kutoka **GWh 6,033.98** Mwaka 2014 na kufikia **GWh 6,227** Mwaka 2015, sawa na ongezeko la takriban **asilimia 3**. Uzalishaji katika vituo vilivyoko nje ya Gridi ya Taifa uliongezeka kutoka **GWh 191.8**

Mwaka 2014 hadi kufikia **GWh 201.44** Mwaka 2015, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 5**.

(ii) **Upatikanaji wa Huduma ya Umeme Nchini**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kiwango cha upatikanaji wa huduma ya umeme *(access level)* kimekuwa kikiongezeka mwaka hadi mwaka. Watanzania waliofikiwa na huduma hiyo wameongezeka kutoka **asilimia 36** mwezi Machi, 2015 hadi kufikia takriban **asilimia 40** mwezi Aprili, 2016. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali za kusambaza umeme nchini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

(iii) **Miradi ya Kuzalisha Umeme**

17. ***Mheshimiwa Spika**,* **nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mradi wa Kinyerezi – I wenye uwezo wa kuzalisha MW 150 kwa kutumia Gesi Asilia umekamilika**. Mradi huu ulizinduliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Oktoba, 2015. Mradi uligharimu **Dola za Marekani milioni 183** sawa na takriban **Shilingi bilioni 315.47** na unamilikiwa na Serikali kwa **asilimia 100** kupitia TANESCO.

18. ***Mheshimiwa Spika**,* katika juhudi za kuongeza uzalishaji umeme, Serikali pia imepanga kuongeza mitambo mingine ya kuzalisha umeme ya ***Kinyerezi – I Extension MW 185***. Mwezi Aprili, 2016 TANESCO na Mkandarasi Kampuni ya Jacobsen Elektro AS wamesaini Mkataba wa utekelezaji wa Mradi huu. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 418.85**. Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi huu ni **Shilingi bilioni 119.04** na umepangwa kukamilika mwishoni mwa Mwaka 2019.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa **Mradi wa Kinyerezi - II MW 240** wa kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia umeanza. Jiwe la msingi la utekelezaji wa Mradi huu liliwekwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwezi Machi, 2016. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 344**, sawa na **Shilingi bilioni 564**, ambapo **Dola za Marekani milioni 292** sawa na **asilimia 85** ni Mkopo kutoka *Japan Bank for International Corporation (JBIC)* na *Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC)* za Japan. Aidha, Serikali imetoa **Shilingi bilioni 110** ikiwa ni **asilimia 15** ya gharama za Mradi wote.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi huo ikiwa ni pamoja na taratibu za ununuzi na usafirishaji wa mitambo na vifaa kutoka Japan. Mradi umepangwa kukamilika Mwezi Desemba, 2019.

**Miradi ya Uzalishaji Umeme Iliyo katika Hatua za Mwisho Kuanza Utekelezaji**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme. Miradi hiyo ni pamoja na Kinyerezi III - MW 300, Rusumo Falls - MW 80, Malagarasi - MW 45 na Kakono - MW 87 na imepangwa kukamilika kabla ya Mwaka 2020.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** **Mradi wa Kinyerezi - III MW 300** utatekelezwa katika eneo la Kinyerezi Mkoa wa Dar es Salaam. Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Mradi utatekelezwa kupitia Kampuni ya SHANGTAN ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya TANESCO (**asilimia 10**) na Shangai Electric Power Company ya China (**asilimia 60**). Aidha, **asilimia 30** ya Hisa zitauzwa kwa Wawekezaji wengine wa Ndani. Gharama ya Mradi ni **Dola za Marekani milioni 389.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 868.2**. Katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha majadiliano ya Mkataba wa kuuziana umeme, kuuza **asilimia 30** ya Hisa kwa Wawekezaji wa Ndani na kuajiri Mkandarasi wa utekelezaji wa Mradi. Mradi utakamilika katika muda wa miezi 36 baada ya kuanza utekelezaji wake.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya ujenzi wa **Mradi wa Rusumo Falls wa kuzalisha umeme wa MW 80** kwa kutumia nguvu za maji kwa ushirikiano wa nchi yetu na nchi za Rwanda na Burundi yamekamilika. Kazi zilizofanyika katika Mwaka 2015/16 ni: kupatikana kwa Wataalamu Washauri Kampuni ya AECOM ya Canada na Kampuni ya ARTELIA ya Ufaransa kwa ajili ya kazi ya kusimamia ujenzi wa mtambo wa kufua umeme na njia ya kusafirishia umeme; na kupatikana kwa Mkuza kwa ajili ya kujenga njia ya kusafirisha umeme.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za kutekeleza Mradi huu zimepatikana kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Gharama za ujenzi wa Mtambo zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 340** sawa na takriban **Shilingi bilioni 757.52**. Katika Mradi huu, mchango wa Tanzania ni mkopo wa **asilimia 100** (**Dola za Marekani milioni 113.33**). Aidha, Rwanda imepata mkopo wa **asilimia 50** (**Dola za Marekani milioni 56.67**) na ruzuku ya **asilimia 50** (**Dola za Marekani milioni 56.67**) na

Burundi imepata ruzuku ya **asilimia 100** (**Dola za Marekani milioni 113.33)**.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi pia utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 98. Gharama ya njia hiyo ya kusafirisha umeme ni **Dola za Marekani milioni 35** sawa na takriban **Shilingi bilioni 77.98**. Kazi zitakazofanyika Mwaka 2016/17 ni kukamilisha taratibu za kupata Wakandarasi wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Fedha za nje zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 5**. Mradi huu utaanza Mwaka 2016/17 na utakamilika Mwaka 2019/20.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya Mradi wa **Malagarasi wa MW 44.8** Mkoa wa Kigoma imekamilika. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 149.5** sawa na **Shilingi bilioni 333.08**. Katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni kukamilisha shughuli za usanifu na kutengeneza nyaraka za zabuni ambapo **Shilingi bilioni 5** zimetengwa. Mradi huu unatarajia kukamilika Mwaka 2019/20.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD) imekamilisha upembuzi yakinifu wa **Mradi wa Kakono wa MW 87** Mkoa wa Kagera. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilomita 38.8 kutoka Kakono hadi Kyaka (Uganda). Miongoni mwa kazi zitakazofanyika ni kumpata Mtaalamu Mshauri wa Mradi, kutayarisha usanifu wa mitambo na kuandaa hati za zabuni. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 379.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 845.27**. Fedha zilizotengwa katika Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi wa Kakono ni **Shilingi bilioni 3**. Mradi huu utakamilika Mwaka 2019/20.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba, 2015 Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iliitisha Mkutano na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutafuta fedha za utekelezaji wa Miradi ya Malagarasi na Kakono. Kufuatia Mkutano huo, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) zimeonesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Kakono na Malagarasi.

**Miradi ya Uzalishaji Umeme ya NDC**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa uzalishaji umeme kutokana na Makaa ya Mawe, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) linaendelea

kusimamia utekelezaji wa **Mradi wa Mchuchuma wa MW 600 na Ngaka MW 400**. Miradi hiyo inasimamiwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

(iv) **Miradi ya Usafirishaji Umeme**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme inayoanzia **Iringa hadi Shinyanga ya Msongo wa *kV 400 (Backbone)*** unaendelea vizuri. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 utekelezaji wa Mradi huo ulifikia wastani wa **asilimia 89**. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 224** sawa na takriban **Shilingi bilioni 387.5**. Mradi utakamilika mwezi Septemba, 2016. Mradi huo utaboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Singida, Shinyanga na Tabora. Aidha, utasaidia kuunganisha Gridi za Taifa za Tanzania, Kenya na Zambia na kuiwezesha Tanzania kushiriki kikamilifu katika biashara ya umeme kupitia *Eastern African Power Pool (EAPP)* na *Southern African Power Pool (SAPP).* Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 20**.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Agosti, 2015 TANESCO ilisaini Mikataba na Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa **Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea** na vituo vya kupozea umeme vya Madaba na Songea vilivyopo Mkoa wa Ruvuma. Aidha, kazi ya kusambaza nguzo za umeme wa Msongo wa kV 33 katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma imeanza.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17 kazi zilizopangwa ni: kukamilisha ujenzi wa njia za usambazaji wa umeme kwa kiwango cha kV 33 na 0.4 katika Wilaya za Ludewa, Mbinga, Namtumbo, Njombe, Songea Mjini na Songea Vijijini; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupozea umeme. Gharama za Mradi huu ni **Krona za Sweden milioni 500** sawa na **Shilingi bilioni 112**. Fedha zilizotengwa na Serikali kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 42**. Mradi umepangwa kukamilika mwezi Desemba, 2017.

**Miradi ya Usafirishaji Umeme Iliyo Katika Hatua za Mwisho Kuanza Utekelezaji**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha umeme unaozalishwa unafika katika maeneo unakohitajika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme zenye uwezo mkubwa, hususan kV 400. Miradi ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwaka 2019/20 ni pamoja na Singida – Arusha – Namanga kV 400, Bulyanhulu – Geita kV

220, Geita – Nyakanazi kV 220, *North – East Grid kV 400* na Somanga – Kinyerezi kV 400.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa **Mradi wa Singida – Arusha - Namanga kV 400** ambao ni sehemu ya Mradi unaounganisha Gridi za Taifa za Zambia, Tanzania na Kenya *(ZTK Interconnector)* umeanza. Mwezi Aprili, 2015 Serikali ilisaini Mkataba wa Mkopo wa **Dola za Marekani milioni 116.7** sawa na **Shilingi bilioni 259.99** na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu. Serikali pia ilisaini Mkataba mwingine wa Mkopo wa Mradi huu wa **Dola za Marekani milioni 98.23** sawa na **Shilingi bilioni 218.85** na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) mwezi Januari, 2016.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika ni: kukamilisha tathmini ya mali za watu watakaopisha Mradi katika Mikoa ya Arusha na Manyara; na kutangazwa kwa zabuni za Wakandarasi wa kujenga vituo vya kupozea umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme. Utekelezaji wa Mradi kwa sehemu ya kutoka Singida hadi Namanga unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 258.82** sawa na **Shilingi bilioni 576.63**. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 23**. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2018/19.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliajiri Kampuni ya Shaker Consulting Group ya Misri kuwa Mshauri Mwelekezi wa kusimamia utekelezaji wa **Mradi wa Bulyanhulu – Geita kV 220** wenye urefu wa kilomita 55. Mshauri huyo pia atasimamia usambazaji umeme katika vijiji 10 Wilayani Geita pamoja na kujenga Kituo cha kupozea umeme Wilayani humo. Kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka 2016/17 ni kumpata Mkandarasi na kuanza kwa utekelezaji wa Mradi. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 23** sawa na takriban **Shilingi bilioni 41**. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huu ni **Shilingi bilioni 6** na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2017/18.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba, 2015 Kampuni ya Lahmeyer International ya Ujerumani iliajiriwa kuwa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia **Mradi wa Geita – Nyakanazi kV 220** wenye urefu wa kilomita 133. Mshauri huyo pia atasimamia ujenzi wa Kituo cha kupozea umeme cha Nyakanazi pamoja na usambazaji wa umeme kwenye vijiji 23 vinavyopitiwa na Mradi. Kazi nyingine zilizokamilika ni Tathmini ya Athari za Kijamii na Mazingira na upimaji wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2018/19.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Gharama za utekelezaji wa Mradi huo ni **Euro milioni 45** sawa na takriban **Shilingi bilioni 81.48**. Mradi huo unafadhiliwa na KfW (Germany), AFD (France), EU na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo ni **Shilingi bilioni 7**. Utekelezaji wa Mradi utaanza mwezi Oktoba, 2016 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2018.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015/16 kazi zilizokamilika katika **Mradi wa North – East Grid kV 400** ni pamoja na Tathmini ya Athari za Kijamii na Mazingira; na tathmini ya mali kwa watu watakaopisha Mradi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Aidha, majadiliano kati ya Serikali yetu na Benki ya Exim ya China kwa ajili ya Mkopo wa **Dola za Marekani milioni 588** sawa na **Shilingi bilioni 1,310** yamekamilika. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 85** ya gharama za Mradi wote na **asilimia 15** itatolewa na Serikali.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi kwa sehemu ya Kinyerezi hadi Chalinze na kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi. Gharama ya Mradi ni **Dola za Marekani milioni 693** sawa na **Shilingi bilioni 1,543.9** ambapo Serikali inachangia **asilimia 15**. Jumla ya fedha zilizotengwa katika Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi huo ni **Shilingi bilioni 16** na utakamilika Mwaka 2019/20.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** TANESCO imesaini Mkataba wa Mkopo wa **Dola za Marekani milioni 150** sawa na **Shilingi bilioni 334.19** na Benki ya Maendeleo ya TIB mwezi Novemba, 2015. Mkopo huo ni kwa ajili ya utekelezaji wa **Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi**. Njia hiyo itakuwa na urefu wa kilomita 198 na pia itahusisha Kituo cha kupozea umeme katika eneo la Somanga Fungu. Mradi huu utaunganisha na kusafirisha hadi Dar es Salaam umeme unaotarajiwa kuzalishwa kutoka Somanga Fungu (MW 350) na Kilwa Energy (MW 320) Mkoani Lindi.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** TANESCO imekamilisha tathmini ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi huu. Hadi mwezi Aprili, 2016 **Shilingi bilioni 26.06** tayari zimelipwa na TANESCO kwa watu 947 katika Wilaya za Ilala na Temeke. Kazi zitakazofanyika kwa Mwaka 2016/17 ni kumpata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa Mradi. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2019. Gharama ya Mradi huo ni **Dola za**

**Marekani milioni 150** sawa na **Shilingi bilioni 334.19**. Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mradi huo ni **Shilingi bilioni 5**. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2019/20.

(v) **Miradi ya Usambazaji Umeme**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa **Mradi wa *Electricity V*** ulikamilika mwezi Desemba, 2015. Mradi huo ulihusu ujenzi wa njia ya kusambaza umeme wa Msongo wa kV 33, kufunga transfoma na kuwaunganishia umeme wateja 8,600 katika Wilaya za Bukombe, Kwimba, Magu, Mbogwe, Misungwi na Sengerema. Wateja waliounganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2016 ni 4,001. Pamoja na kuwa Mradi umekamilika kulingana na Mkataba wa Mkopo kutoka AfDB, TANESCO itaendelea na kazi ya kuwaunganishia umeme wateja waliobaki.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu pia ulihusu ukarabati wa Vituo vya kupozea umeme vya Ilala na Sokoine katika Jiji la Dar es Salaam na upanuzi wa Kituo cha kupozea umeme cha Njiro Mkoani Arusha. Mradi ulitekelezwa na Serikali kupitia Mkopo uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mradi uligharimu Jumla ya ***Unit of Account (UA)*** **milioni 32.25** sawa na takriban **Shilingi bilioni 101.31**. Kati ya fedha hizo ***UA*** **milioni 28.68** sawa na **asilimia 89** ni Mkopo kutoka AfDB na ***UA*** **milioni 3.57** sawa na **asilimia 11** zilitolewa na Serikali yetu.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** **Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini *(REA Turnkey Phase II)*** inaendelea kutekelezwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa Vituo sita (6) vya umeme wa kV 11/33 katika Miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru; ujenzi wa njia za kusambaza umeme zenye urefu wa takriban kilomita 15,000 za Msongo wa kV 33; ujenzi wa Vituo vidogo 3,100 vya kupozea na kusambaza umeme vyenye uwezo wa kV 33/0.4/0.23; na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme wenye urefu wa kilomita 7,000. Kwa ujumla hadi kufikia Aprili, 2016 utekelezaji wa Mradi wa *REA Turnkey Phase II* umefikia **asilimia 85**.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imekamilisha kazi ya kuunganisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya 4 za Buhingwe, Kakonko na Uvinza zilizopo katika Mkoa wa Kigoma na Nyasa iliyopo katika Mkoa wa Ruvuma. Kuanzia Julai, 2015 hadi Aprili, 2016 idadi ya wateja waliounganishiwa umeme na REA pamoja na TANESCO ni 220,128

sawa na **asilimia 88** ya lengo la kuunganisha wateja 250,000 ifikapo Juni, 2016.

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2016/17 Serikali itafanya tathmini ya kina ya Awamu ya Kwanza na ya Pili ya utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini. Lengo la tathmini hiyo ni kuboresha maandalizi na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini *(REA Turnkey Phase III)*. Pamoja na tathmini hiyo, masuala yatakayozingatiwa katika Awamu ya Tatu ni kupeleka umeme: kwenye vijiji ambavyo havikupata umeme katika awamu ya kwanza na ya pili; kwenye viwanda vidogo vya uzalishaji mali; na katika shule za sekondari, hospitali, zahanati, vituo vya afya, pampu za maji na maeneo mengine muhimu ya huduma za jamii. Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini itaanza Mwaka 2016/17 na kukamilika Mwaka 2018/19.

48. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza wigo wa upatikanaji umeme vijijini, Serikali imeongeza Bajeti ya Maendeleo ya fedha za ndani kwa REA kutoka **Shilingi bilioni 357.12** kwa Mwaka 2015/16 hadi **Shilingi bilioni 534.4** kwa Mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la **asilimia 50**. Ongezeko hilo ni katika kutekeleza **Ibara ya 43 C(i) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020**. Aidha, fedha za nje zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huo ni **Shilingi bilioni 53.21** sawa na **asilimia 9** na hivyo kufanya Jumla ya Bajeti yote ya REA kwa Mwaka 2016/17 kuwa **Shilingi bilioni 587.61**. Vilevile, REA ipo katika taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayetekeleza Mradi wa kusambaza umeme kwenye vijiji 121 inakopita njia kuu ya umeme ya Iringa hadi Shinyanga *(Backbone).* Taratibu hizo za ununuzi zitakamilika ifikapo Mwezi Desemba, 2016.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza kasi ya kusambaza umeme vijijini, REA imeanza miradi ya kusambaza umeme kwenye vijiji vinavyopitiwa na miundombinu ya umeme ya Msongo wa kV 11 na 33 *(Underline Distribution Transformers)*. Mradi huu unahusisha kufunga transfoma na kusambaza umeme kupitia miundombinu ya kusambaza umeme ya Msongo wa kV 0.4/0.23. Tathmini ya Awamu ya Kwanza ya Mradi imekamilika katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Mara, Mbeya, Pwani na Tanga. Katika Mwaka 2016/17, REA inatarajia kuanza kutekeleza Mradi huu baada ya taratibu za kuwapata Wakandarasi kukamilika Mwezi Desemba, 2016. Mradi huu utagharimu Jumla ya **Shilingi bilioni 58.4**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 28.7** sawa **asilimia 49** ni fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini na **Shilingi bilioni 29.7** sawa na **asilimia 51** ni fedha kutoka Serikali ya

Sweden na Norway. Mradi utaanza kutekelezwa Mwezi Januari, 2017 na utakamilika baada ya miezi 18.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** TANESCO imeendelea kutekeleza **Mradi wa kupeleka umeme katika Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngara kupitia Programu ya ORIO**. Kwa upande wa Wilaya za Biharamulo na Ngara utekelezaji umefikia **asilimia 65**. Ufungaji wa jenereta zenye uwezo wa Jumla ya MW 2.5 kwa kila Wilaya umeanza mwezi Aprili, 2016. Vilevile, ujenzi wa njia za kusambaza umeme umeanza mwezi Februari, 2016.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha mchango wake wa **Shilingi bilioni 22** kwa ajili ya Mradi huu baada ya kutolewa kwa **Shilingi bilioni 11.5** mwezi Machi, 2016 ili kupeleka umeme Wilaya ya Mpanda. Kufuatia kutolewa kwa fedha hizo, utekelezaji wa Mradi ulianza mwezi Aprili, 2016 kwa Mkandarasi ZWART Tekniek B.V kutoka Uholanzi kuagiza majenereta. Gharama za Mradi ni **Euro milioni 33.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 81.5**. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ufalme wa Uholanzi. Upelekaji umeme katika Wilaya za Biharamulo na Ngara unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2016 na Wilaya ya Mpanda utakamilika mwezi Juni, 2017.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa **Mradi wa *Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)*** unaendelea katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro. Jumla ya Vituo 19 vya kusambaza umeme wa Msongo wa kV 33/11 vitakarabatiwa. Aidha, ujenzi wa njia za usambazaji umeme za Msongo wa kV 33 zenye urefu wa kilomita 107 zinajengwa. Vilevile, njia za usambazaji umeme wa Msongo wa kV 11 zenye urefu wa kilomita 50 zitajengwa. Jumla ya transfoma 65 za kV 33/0.4 zitafungwa. Katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2016.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya **Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II)** ulianza mwezi Oktoba, 2015. Mradi huu unahusu ujenzi wa mifumo ya Umeme wa Jua katika Wilaya nane (8) za Biharamulo (Kagera), Bukombe na Chato (Geita), Kasulu na Kibondo (Kigoma), Namtumbo na Tunduru (Ruvuma) na Sikonge (Tabora). Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 18** sawa na **Shilingi bilioni 40.1** ambazo ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika Wilaya hizo kupitia REA katika Mwaka 2016/17 na utakamilika Mwaka 2017/18.

(vi) **Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati na Mwelekeo wa Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme *(Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap).* Katika Mwaka 2015/16 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha utayarishaji wa Mikataba Kifani ya Kuuziana Umeme *(Model Power Purchase Agreement -MPPA)* mwezi Agosti, 2015; kukamilisha uandaaji wa *Grid Codes;* na mwongozo wa tozo kwa kampuni moja kutumia miundombinu ya kampuni nyingine kusafirisha umeme *(transmission wheeling charges rules)*.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango huo ikiwa ni pamoja na zoezi la tathmini ya mali za TANESCO; tathmini ya rasilimali watu inayohitajika katika Sekta Ndogo ya Umeme, Mafuta na Gesi Asilia; na ukaguzi wa mifumo ya kompyuta ya TANESCO.

(vii) **Punguzo la Viwango vya Bei za Umeme**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** **nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetekeleza ahadi yake ya kupunguza bei za umeme**. Kuanzia tarehe 01 Aprili, 2016 Serikali imepunguza bei ya umeme kwa kati ya **asilimia 1.5** na **2.4**. Serikali pia imeondoa tozo ya kuwasilisha maombi ya kuunganishiwa umeme *(application fees)* ya **Shilingi 5,000** na tozo ya huduma ya mwezi *(service charge)* ya **Shilingi 5,520** kwa Wateja wa Umeme kwa Daraja la T1 na D1, ambao wengi wao ni wa majumbani. Hatua hii itawasaidia watumiaji wadogo wa umeme mijini na vijijini kumudu gharama hizo, hivyo kuboresha shughuli za kijamii na kiuchumi.

(viii) **Kuboresha Huduma za Wateja kwa Kuanzisha Ofisi Ndogo za TANESCO**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini, Serikali kupitia TANESCO ina mpango wa kufungua Ofisi mpya 20 zenye hadhi ya Wilaya na Ofisi Ndogo *(sub-offices)* 46 katika maeneo mbalimbali nchini ili kuboresha huduma za TANESCO kwa wateja. Ujenzi wa Ofisi hizo unakadiriwa kugharimu **Shilingi bilioni 43.2** kwa kutumia vyanzo vya ndani vya Shirika. Aidha, endapo TANESCO itatumia majengo ya kupanga, gharama zinakadiriwa kuwa **Shilingi milioni 948** kwa Mwaka. Vigezo vitakavyotumika kuanzisha Ofisi mpya ni: urefu wa njia za umeme katika eneo husika; idadi ya transfoma na wateja

waliopo; mahitaji ya juu ya umeme; na umbali kutoka Ofisi ya TANESCO ya Mkoa au Wilaya.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini, Mwaka 2014 TANESCO ilianzisha Kampuni Tanzu ya Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited (TCPCO). Kampuni hiyo imeainisha Kanda nne kwa ajili ya kujenga viwanda vya kutengeneza nguzo za zege nchini. Kanda hizo ni Mashariki, Kaskazini, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini Magharibi. Baada ya kukamilisha maandalizi na ujenzi wa viwanda hivyo, TCPCO inatarajia kuanza uzalishaji wa nguzo za zege Mwaka 2016/17.

**Kuboresha Miundombinu ya Umeme Jijini Dar es Salaam**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Kituo cha kupozea umeme cha kV 132/33/MVA 2x45 City Centre umekamilika. Kituo kipo katika hatua za majaribio na kinatarajiwa kufunguliwa rasmi Mwezi Juni, 2016. Aidha, ujenzi wa Kituo cha kuongoza mifumo ya usambazaji umeme katika msongo wa kV 33 na kV 11 *(Distribution SCADA)* umekamilika na Kituo kipo kwenye majaribio. Vilevile, ujenzi wa njia ya umeme chini ya ardhi kwa msongo wa kV 132 kutoka Makumbusho kwenda City Centre umekamilika. Miongoni mwa manufaa ya Mradi huu ni kuwezesha wateja kupata huduma bora za umeme. Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Finland na Japan kwa gharama za **Shilingi bilioni 123** sawa na **Dola za Marekani milioni 55.21**.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mradi huu utaendelea katika Mwaka 2016/17 kwa kukamilisha ujenzi wa njia ya umeme chini ya ardhi kwa msongo wa kV 132 kutoka City Centre hadi Shule ya Sekondari Jangwani na ujenzi wa njia ya kV 132 kutoka Ilala hadi Shule ya Sekondari Jangwani.

(ix) **Uendelezaji wa Nishati Jadidifu**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia **maporomoko madogo ya maji *(mini – hydro)***. Katika Mwaka 2015/16 Miradi iliyokamilika ni Andoya (Mbinga), Darakuta (Manyara), Tulila (Songea) na Yovi (Kilosa) na ina uwezo wa kuzalisha Jumla ya MW 6.6. Aidha, katika Mwaka 2016/17 Serikali itasimamia Miradi inayoendelea yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 10.24 na

mingine yenye Jumla ya MW 58.6 ambayo ipo katika hatua za mwisho za kuanza utekelezaji.

**Bayogesi *(Biogas)***

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015/16, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Uendelezaji wa Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)* iliendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kujenga Mitambo ya Bayogesi nchini. Hadi mwezi Mei, 2016 Jumla ya Mitambo 14,000 ilijengwa katika ngazi ya kaya ikilinganishwa na Mitambo 12,000 kwa Mwaka 2014/15. Programu hiyo imewezesha wananchi 84,000 kutumia nishati hiyo kwa ajili ya kupikia na kupata mwanga. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwaka 2017 CAMARTEC itakuwa imejenga Jumla ya Mitambo 21,000.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari, 2016 Serikali pia imeanza kutekeleza Mradi wa matumizi ya Bayogesi majumbani kupitia REA. Mradi unahusisha ujenzi wa mifumo 10,000 ya Bayogesi kwenye Mikoa yote ya Tanzania Bara katika kipindi cha miaka miwili kuanzia Mwaka huu. Mradi unafadhiliwa na Serikali ya Norway kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.2**. Lengo la Serikali ni kuhamasisha matumizi ya Bayogesi majumbani ili kupunguza matumizi ya kuni, mkaa na aina nyingine za tungamotaka zinazosababisha uharibifu wa mazingira.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa umeme kwa kutumia bayogesi ni moja ya vyanzo vinavyotarajiwa kuchangia ongezeko la umeme katika Gridi ya Taifa. Kampuni ya Mkonge Energy Systems inatarajia kutumia majitaka ya mkonge *(sisal waste water)* kuzalisha Jumla ya MW 1.5 katika mashamba ya mkonge yaliyoko kwenye vijiji vya Magoma (kW 500), Mwelya (kW 500) na Usambara (kW 500) vilivyopo Wilaya ya Korogwe.

**Jotoardhi *(Geothermal)***

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015/16, Serikali kupitia Kampuni Tanzu ya TANESCO ya Uendelezaji wa Jotoardhi *(Tanzania Geothermal Development Company Limited - TGDC),* imekamilisha utafiti na kuthibitisha sehemu tatu katika eneo la Ziwa Ngozi, Mbeya zitakazochorongwa visima virefu ili kutathmini kiasi cha mvuke kinachoweza kuzalisha umeme. Vilevile, mwezi Desemba, 2015 Serikali ilisaini Mkataba wa Ushirikiano *(Partnership Agreement)* na Serikali ya Iceland kupitia Shirika la Maendeleo la Iceland (ICEIDA) kwa lengo la kuzalisha umeme kutokana na jotoardhi.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Serikali kupitia TGDC itachoronga visima virefu vitatu katika eneo la Ziwa Ngozi, Mbeya kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 38** sawa na **Shilingi bilioni 84.66**. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali, *Global Risk Mitigation Fund (GRMF)* na *Investment Climate Fund (CIF)* kupitia *Scaling-Up Renewable Energy Programme (SREP)*. TGDC pia itaendeleza utafiti katika maeneo ya Kisaki (Morogoro), Luhoi (Pwani), Mbaka (Mbeya), Mlima Meru na Ziwa Natron (Manyara) kwa kushirikiana na *Federal Institute for Geosciences and Natural Resources (BGR)*, *Global Risk Mitigation Fund (GRMF)*, *Icelandic International Development Agency (ICEIDA)* na *United Nations Environment Programme (UNEP)*.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha Miongozo, Mipango na Sheria ya kuendeleza Jotoardhi nchini. Katika Mwaka 2016/17, Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Jotoardhi ni **Shilingi bilioni 28**. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 2** sawa na **asilimia 7** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 26** sawa na **asilimia 93** ni fedha za nje.

**Nishati ya Upepo na Jua *(Wind and Solar Energy)***

68. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya kubainisha maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati ya jua na upepo zimekamilika. Taarifa za utafiti zilikusanywa na kutumika kuandaa Ramani zinazoonesha maeneo yanayofaa kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo hivyo. Lengo la kuwa na Ramani hizo ni kuhamasisha uwekezaji kwenye vyanzo vya kufua umeme kutokana na nishati mbadala au jadidifu.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** kama sehemu ya utekelezaji wa **Ibara ya 45(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2015 – 2020)** Serikali imepanga kupeleka umeme maeneo yasiyofikiwa kwa urahisi na Umeme wa Gridi kwa kutumia mifumo midogo ya Umeme wa Jua. Katika Mwaka 2016/17, Serikali inapanga kupeleka umeme katika maeneo ya visiwa vidogo katika Ziwa Victoria na eneo la Kisiwa cha Mafia kwa kutumia mifumo midogo ya Umeme wa Jua. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hizo ni **Shilingi bilioni 6.5**.

**Tungamotaka *(Biomass)***

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Januari, 2016 Wizara ilifanya majadiliano na Kampuni za kuzalisha sukari za Kagera, Kilombero, Mtibwa na TPC kwa lengo la kuongeza uzalishaji umeme kwa kutumia mabaki ya miwa

*(bagasse)*. Endapo umeme mwingi utazalishwa na viwanda hivyo, ziada itaweza kuuzwa kwa TANESCO. Aidha, viwanda hivyo vimeshauriwa kupunguza matumizi ya mvuke katika uzalishaji wa sukari ambapo wataweza kuokoa kiasi cha MW 2 zinazoweza kuuzwa TANESCO.

(x) **Matumizi Bora ya Nishati *(Energy Efficieny)***

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ)* imekusanya takwimu za matumizi ya nishati kwenye viwanda vikubwa *(baseline information)*. Takwimu hizi zitasaidia kuandaa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati Nchini *(Energy Efficiency Action Plan)*. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na GIZ ilifanya *Energy Audit* ili kuhamasisha matumizi bora ya nishati katika Mamlaka za Maji za Morogoro na Singida kwa lengo la kupunguza matumizi ya umeme yasiyo ya lazima. Matokeo ya ukaguzi uliofanyika yalionesha kuwa uniti 1,031,570 na uniti 786,458 za umeme zinaweza kuokolewa kwa mwaka kwenye Mamlaka za Maji za Morogoro na Singida, sawia kwa kutekeleza mipango ya matumizi bora ya nishati.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na *GIZ* itakamilisha na kuanza utekelezaji wa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati. Vilevile, Serikali itafanya utafiti wa kiasi cha nishati kinachoweza kuokolewa katika Ofisi za Serikali na Viwandani ikiwa matumizi bora ya nishati yatazingatiwa.

## SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

(i) ***Shughuli za Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia***

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Dodsal imekamilisha tathmini ya kiasi cha Gesi Asilia kilichogunduliwa katika Kisima cha Mambakofi – I kwenye Kitalu cha Ruvu Mkoa wa Pwani. Tathmini hiyo inaonesha uwepo wa Gesi Asilia kiasi cha futi za ujazo trilioni *(TCF)* 2.17, hivyo kufanya Gesi Asilia iliyogunduliwa nchini hadi mwezi Mei, 2016 kufikia **TCF 57.25** ikilinganishwa na **TCF 55.08** zilizokuwepo mwezi Aprili, 2015. Kati ya kiasi hicho **TCF 47.13** zipo kwenye kina kirefu baharini na **TCF 10.12** zipo nchi kavu.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba, 2015 Kampuni ya Pan African Energy *(PAET)* ilikarabati Visima vya SS – 5, SS – 7 na SS – 9 pamoja na kuchoronga Kisima kipya cha SS – 12 mwezi Januari, 2016. Shughuli hizo zimeongeza uzalishaji wa Gesi Asilia kutoka Songo Songo kutoka futi za

ujazo milioni *(mmscfd)* 105 kwa siku hadi futi za ujazo milioni *(mmscfd)* 190 kwa siku.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeendelea kusimamia kazi ya utafutaji Mafuta na Gesi Asilia katika maeneo mbalimbali nchini. Katika Mwaka 2015/16, Shirika lilikusanya takwimu za kijiolojia kwa kutumia ndege - *Airborne Gravity Gradiometer (AGG)* na *Full Tensor Gradiometry (FTG)* katika maeneo ya Eyasi-Wembere (Manyara), Ziwa Tanganyika Kaskazini (Kigoma), Songo Songo Magharibi na Mandawa (Lindi) kwa lengo la kuongeza thamani ya maeneo hayo. Katika Vitalu 4-1B na 4-1C vilivyopo katika kina kirefu baharini, TPDC ilikamilisha tathmini ya awali ya kijiolojia na kijiofizikia kwa kukusanya takwimu za Mitetemo ya 2D katika maeneo hayo. TPDC inaendelea kufanya uchambuzi wa takwimu hizo ili kujiridhisha kama maeneo husika yana dalili za kuwa na Mafuta au Gesi Asilia. Kazi hiyo itakamilika mwishoni mwa Mwezi Juni, 2016.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti, 2015 Kampuni ya Maurel & Prom pamoja na Wabia wake walifanikiwa kuchoronga Kisima MB – 4 katika Kitalu cha Mnazi Bay (Mtwara). Aidha, Kisima hicho kipya pamoja na Visima vya MB – 2, MB – 3 na MSX – 1 viliunganishwa kwenye Mtambo wa kusafisha Gesi Asilia katika eneo la Madimba (Mtwara). Hadi sasa Gesi Asilia iliyopo katika Kitalu hicho inakadiriwa kufikia futi za ujazo trilioni *(TCF)* 5 na uzalishaji wake ni wastani wa futi za ujazo milioni 59 kwa siku.

(ii) ***Miundombinu ya Kusafisha na Kusafirisha Gesi Asilia***

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara kupitia Lindi hadi Dar es Salaam (kilomita 542) pamoja na Mitambo ya kusafisha Gesi Asilia katika maeneo ya Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi). Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Oktoba, 2015. Kukamilika kwa Mradi huo kumeongeza mchango wa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia kufikia **asilimia 49**. Uzalishaji wa umeme kwa kutumia Gesi Asilia umewezesha gharama za uzalishaji umeme nchini kupungua kutoka wastani wa **Shilingi 262 hadi 229** kwa uniti moja ya umeme.

**Mradi wa Miundombinu ya *Liquefied Natural Gas (LNG)***

78. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba, 2015 TPDC ilikamilisha taratibu za kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Mitambo ya kusindika Gesi Asilia *(LNG*)

katika Kijiji cha Likong'o (Lindi). TPDC ilipewa Hati Miliki na Serikali kwenye eneo la ukubwa wa Hekta 2,071 kwa ajili ya kujenga Mitambo hiyo. Washirika wakubwa katika Mradi huu ni pamoja na TPDC, Kampuni za BG/Shell, Statoil, ExxonMobil, Pavillion na Ophir. Katika Mwaka 2016/17, kazi zitakazofanyika ni pamoja na upimaji wa eneo la kujenga Mitambo ya Mradi wa LNG, kupata vibali vya kuingiza kwenye Ramani za Mipango Miji michoro ya LNG, maeneo ya viwanda *(Industrial Parks)* na uwanja wa ndege. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo ni **Shilingi milioni 800**.

**Mradi wa Usambazaji Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara**

79. ***Mheshimiwa Spika,*** TPDC ilikamilisha upembuzi yakinifu wa awali, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza Gesi Asilia katika Miji ya Kilwa, Lindi na Mtwara. TPDC pia imeajiri Kampuni ya KIMPHIL Konsult (T) Limited kuwa Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi wa kina kuhusu Mradi huu. Mradi utahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza Gesi Asilia kwa njia ya Bomba *(Piped Natural Gas – PNG)* na iliyoshindiliwa *(Compressed Natural Gas - CNG)*. Lengo la Mradi huu ni kusambaza Gesi Asilia kwa ajili ya mitambo ya kuzalisha umeme, matumizi majumbani, viwandani, kwenye magari na taasisi mbalimbali. Gharama za awali za Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 10** sawa na takriban **Shilingi bilioni 22.3**. Katika Mwaka 2016/17 fedha zilizotengwa ni **Shilingi milioni 700**.

**Usambazaji wa Gesi Asilia Jijini Dar es Salaam**

80. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la Mradi huu ni kujenga Mtandao wa kusambaza Gesi Asilia kwa njia ya Mabomba na *CNG.* Kwa hatua za awali Mradi utaunganisha wateja 30,000 wa majumbani na kujenga vituo 15 vya kujazia Gesi Asilia kwenye magari. Kazi za upembuzi yakinifu na uandaaji wa michoro kwa ajili ya Mradi zimekamilika. Gharama za Mradi ni takriban **Dola za Marekani milioni 150** sawa na **Shilingi bilioni 334.19**. Serikali kupitia Wizara ya Fedha, inafanya majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kupata fedha za kutekeleza Mradi huu. Katika Mwaka 2016/17 fedha zilizotengwa ni **Shilingi bilioni 5**.

(iii) **Mradi wa Uzalishaji Mbolea kwa kutumia Gesi Asilia**

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imesaini Mkataba wa Ubia na Kampuni ya Ferrostaal ya Ujerumani mwezi Septemba, 2015 kwa ajili ya

kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea. Mradi huu utagharimu **Dola za Marekani bilioni 1.98** sawa na **Shilingi bilioni 4,411.24** na ujenzi unatarajiwa kuchukua takriban miaka mitatu na nusu. Kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha Mbolea ya Urea tani 3,850 kwa siku na kitatumia Gesi Asilia kiasi cha futi za ujazo Trilioni 1 kwa miaka 20. Vilevile, mchango wa TPDC katika Mradi huu ni ardhi yenye eneo la ukubwa wa Hekari 425 lililopo Kilwa Masoko (Lindi) ambapo kiwanda kitajengwa. Kwa mujibu wa Mkataba wa utekelezaji wa Mradi huu, TPDC itaruhusiwa kumiliki hadi **asilimia 40** ya Hisa za Kampuni itakayojenga kiwanda hiki.

(iv) **Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Masuala ya Petroli**

82. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia Sheria ya Petroli ya Mwaka, 2015 Wizara inaendelea na taratibu za kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Masuala ya Petroli *(Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA).* Mwezi Februari, 2016 Serikali imeunda Kamati Maalum *(Interim Committee)* ya kutekeleza majukumu ya PURA katika kipindi cha mpito pamoja na kuratibu shughuli mbalimbali zinazolenga kuifanya PURA kuwa chombo kamili cha udhibiti ifikapo mwezi Julai, 2016.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuandaa Mpango Kazi wa Uanzishwaji wa PURA; kuandaa Muundo na Kazi za Mamlaka *(Organisational Structure and Scheme of Service);* kuandaa Rasimu ya Mpango Mkakati *(Draft Strategic Plan)*; kuandaa Bajeti pamoja na Mpango wa upatikanaji wa rasilimali fedha; na kuandaa Rasimu za Miongozo na Kanuni *(Rules and Regulations)* mbalimbali zitakazowezesha PURA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Bodi ya Wakurugenzi ya PURA itateuliwa Mwezi Julai, 2016.

84 ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na majukumu mengine PURA itakagua Mikataba na kuchambua masuala ya kiuchumi katika kuingia Mikataba ya utafutaji na ugawanaji mapato yatokanayo na shughuli za Mafuta na Gesi Asilia; itasimamia masuala ya ushiriki wa Watanzania katika shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia; na kufuatilia na kutathmini shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015 inaipa PURA mamlaka ya kukagua au kuagiza kufanyika ukaguzi wa vyanzo vya mapato ya Serikali katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

### (v) Wakala wa Uagizaji wa Mafuta ya Petroli kwa Pamoja

85. ***Mheshimiwa Spika,*** **nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekamilisha uanzishwaji wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja** *(Petroleum Bulk Procurement Agency – PBPA)* mwezi Januari, 2016. Wakala huo pamoja na kazi nyingine unatekeleza majukumu ya iliyokuwa Kampuni Binafsi ya kuratibu Uagizaji wa Mafuta ya Petroli kwa Pamoja *(Petroleum Importation Coordinator Limited - PICL).* Kampuni hiyo ilikuwa inamilikiwa na Kampuni binafsi za uagizaji na usambazaji wa mafuta ya petroli nchini. Lengo la kuanzisha Wakala huu ni kuongeza ufanisi katika shughuli za uagizaji mafuta ya petroli nchini.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa majukumu ya Wakala huu ni kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta ya Petroli kwa Pamoja *(Petroleum Bulk Procurement System - BPS)* na kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya petroli ya kutosha wakati wote nchini. Katika Mwaka 2016/17, Wakala utaanza pia kuratibu uagizaji wa *Liquefied Petroleum Gas - LPG* pamoja na mafuta mazito *(Heavy Fuel Oil - HFO)* kupitia mfumo wa *BPS*.

**Uagizaji wa Mafuta ya Petroli**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** kama ambavyo Serikali iliahidi katika Bunge lako la Bajeti ya Mwaka 2015/16, Bandari ya Tanga ilianza kupokea mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji Mafuta ya Petroli kwa Pamoja *(BPS)* kuanzia mwezi Julai, 2015. Katika kipindi cha Januari na Desemba, 2015 Jumla ya lita **bilioni 5.16** za mafuta ya petroli ziliingizwa nchini kupitia Bandari za Dar es Salaam (lita bilioni 4.25) na Tanga (lita milioni 91.27). Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 12** ikilinganishwa na **lita bilioni 4.63** zilizoingizwa Mwaka 2014. Kati ya mafuta hayo, **lita bilioni 3.1** sawa na **asilimia 60** yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na **lita bilioni 2.06** sawa na **asilimia 40** yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani yameongezeka kwa **asilimia 9** kutoka **lita bilioni 2.84** Mwaka 2014 hadi lita **bilioni 3.10** Mwaka 2015. Aidha, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya nchi jirani yameongezeka kwa **asilimia 15** kutoka **lita bilioni 1.79** Mwaka 2014 hadi **lita bilioni 2.06** Mwaka 2015. Ongezeko hilo linatokana na kukua kwa mahitaji ya Mafuta ndani ya nchi pamoja na nchi jirani kuongeza uagizaji wa Mafuta kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

(vi) **Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soka la Dunia**

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Januari, 2015 bei ya Mafuta katika Soko la Dunia ziliendelea kushuka na kufikia wastani wa **Dola za Marekani 38** kwa pipa la Mafuta Ghafi kwa Mwezi Desemba, 2015. Aidha, wastani wa bei ya Mafuta yaliyosafishwa kwa kipindi cha kati ya Mwezi Januari na Desemba, 2015 ulikuwa kama ifuatavyo: Petroli kutoka **Dola za Marekani 669** hadi **Dola za Marekani 437** kwa tani; Dizeli kutoka **Dola za Marekani 570** hadi **Dola za Marekani 335** kwa tani; na Mafuta ya Taa/Ndege kutoka **Dola za Marekani 570** hadi **Dola za Marekani 363** kwa tani ambayo ni sawa na punguzo la **asilimia 35** kwa Petroli, **asilimia 41** kwa dizeli na **asilimia 39** kwa Mafuta ya Taa/Ndege, sawia.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Bei ya Mafuta katika Soko la Ndani hutegemea bei ya mafuta ya petroli katika Soko la Dunia pamoja na Thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na Dola ya Marekani. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2015 wastani wa bei za mafuta katika Soko la Ndani kwa lita ilikuwa: Petroli **Shilingi 1,973**, Dizeli **Shilingi 1,808** na Mafuta ya Taa **Shilingi 1,739** ikilinganishwa na wastani **Shilingi 2,186** kwa Petroli, **Shilingi 2,082** kwa Dizeli na **Shilingi 2,030** kwa Mafuta ya Taa kwa kipindi kama hicho katika Mwaka 2014.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA iliendelea kusimamia shughuli za uagizaji wa *LPG* nchini. Kati ya Januari na Desemba, 2015 Jumla ya tani 70,061 ziliagizwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini ikilinganishwa na tani 65,611 Mwaka 2014, sawa na ongezeko la **asilimia 7.** Ongezeko hilo linatokana kuongezeka kwa uelewa kuhusu manufaa ya matumizi ya LPG, kuboreshwa kwa miundombinu ya kuhifadhi, kujaza mitungi na kusambaza *LPG.* Katika Mwaka 2016/17 EWURA itaendelea kuisimamia Sekta Ndogo ya Mafuta Nchini.

(vii) **Hisa za Serikali katika Kampuni za PUMA, TAZAMA na TIPER**

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia Hisa zake katika Kampuni za PUMA Energy Tanzania Limited – **asilimia 50**; Tanzania - Zambia Pipeline Limited (TAZAMA – **asilimia 30**); na Tanzania International Petroleum Reserve *(*TIPER – **asilimia 50***).* Kampuni hizo zimekamilisha hesabu za Mwaka 2014, ambapo Serikali imepata Gawio la **Shilingi bilioni 3** kutoka PUMA. Kampuni ya TIPER ilipata faida ya **Dola za Marekani milioni 11.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 25.6**,

ambapo wanahisa walikubaliana badala ya kutoa Gawio waziwekeze katika kuboresha miundombinu ya hifadhi ya mafuta kutoka lita za ujazo 71,000 hadi lita za ujazo 212,000. Aidha, Kampuni ya TAZAMA haikutoa Gawio kwa kuwa haikupata faida katika kipindi husika. Katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuzisimamia Kampuni hizo ili kuongeza ufanisi na kupata Gawio kubwa zaidi.

(viii) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Aprili, 2016 Serikali ya Tanzania ilisaini Makubaliano ya Awali *(MoU)* na Serikali ya Uganda kwa ajili ya ujenzi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Bandari ya Tanga, Tanzania. Bomba hilo litakuwa na urefu wa kilomita 1,443 ambapo kati ya hizo kilomita 1,115 zitakuwa upande wa Tanzania. Bomba hilo litakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa 200,000 ya Mafuta Ghafi kwa siku.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Tanzania, utekelezaji wa Mradi huu utakuwa na manufaa mbalimbali yakiwemo: kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato kupitia Bandari ya Tanga na tozo ya kupitisha Mafuta Ghafi kwenye Bomba; kuongezeka kwa uwekezaji wa fedha za kigeni; na fursa za ajira za kudumu kwa Watanzania takriban 1,000 na 10,000 za muda wakati wa ujenzi. Majadiliano ya utekelezaji wa Mradi huu kati ya Serikali za Tanzania, Uganda, TPDC pamoja na Kampuni za TOTAL (France), CNOOC (China) na Tullow (UK) yameanza.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali ya Uganda imealika nchi za Burundi, Kenya, Rwanda na Tanzania kushiriki katika uwekezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusafisha Mafuta Ghafi *(Oil Refinery)* nchini Uganda. Kila nchi imepewa fursa ya kushiriki kwa kununua **asilimia 8** ya Hisa za Mradi ambazo makisio yake ya awali ni **Dola za Marekani milioni 150.4** sawa na **Shilingi bilioni 335.08**. Katika Mradi huo, Sekta Binafsi pia imekaribishwa kushiriki. Serikali ya Tanzania imeridhia ushiriki katika uwekezaji kwenye Kiwanda hicho cha Kusafisha Mafuta Ghafi.

(ix) **Sera na Sheria katika Sekta ya Nishati**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015/16, Serikali imekamilisha Sera ya Taifa ya Nishati, 2015 na Sheria ya Petroli, 2015. Lengo la kupitisha Sera na Sheria hizo ni kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Nishati nchini.

Katika Mwaka 2016/17, Kanuni na Miongozo mbalimbali itaandaliwa kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa Sera na Sheria hizo.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeandaa Miongozo ya Uanzishwaji wa Miradi ya Umeme kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008 - *The Electricity (Initiation of Power Procurement) Rules 2014*. Lengo la Mwongozo ni kuhakikisha kuwa uwekezaji katika Miradi ya Umeme unafanyika kwa tija na kuleta unafuu kwa wananchi na uchumi wa nchi yetu.

**SEKTA YA MADINI**

**Uzalishaji na Biashara ya Madini**

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015 Jumla ya wakia milioni 1.37 za dhahabu, wakia 497,152 za fedha na ratili milioni 13.76 za shaba zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka Migodi Mikubwa ya dhahabu ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi, North Mara, Stamigold Biharamulo na New Luika. Jumla ya thamani ya madini hayo ni **Dola za Marekani bilioni 1.63** ikilinganishwa na **Dola za Marekani bilioni 1.66** kwa Mwaka 2014, sawa na pungufu kwa takriban **asilimia 2**. Mrabaha uliolipwa Serikalini kutokana na madini hayo ni **Dola za Marekani milioni 63.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 140.8**.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa madini ya Tanzanite, Jumla ya gramu milioni 2.4 za Tanzanite ghafi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.48** zilizalishwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi na Kampuni ya TanzaniteOne. Mrabaha uliolipwa Serikalini kutokana na mauzo ya Tanzanite ni Jumla ya **Dola za Marekani 223,979**. Vilevile, Jumla ya karati 191,407 za madini ya almasi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 53.34** zilizalishwa na kuuzwa na Mgodi wa Mwadui ambapo Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 2.30** ulilipwa Serikalini.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** biashara ya madini Duniani imeendelea kukumbwa na mtikisiko kutokana na kushuka kwa bei kulikoathiri uwekezaji kwenye Sekta hiyo. Bei ya wakia moja ya dhahabu imeshuka kutoka **Dola za Marekani 1,266.19** Mwaka 2014 hadi kufikia wastani wa **Dola za Marekani 1,160.12** Mwaka 2015, sawa na upungufu wa **asilimia 8**. Bei ya shaba ilishuka kwa **asilimia 20** kutoka wastani wa **Dola za Marekani 3.11** kwa ratili Mwaka 2014 hadi **Dola za Marekani 2.50** Mwaka 2015, huku bei ya fedha ikishuka kwa **asilimia 18** kutoka **Dola za Marekani 19.08** Mwaka 2014 hadi **Dola za Marekani 15.70** kwa wakia Mwaka

2015. Hali hiyo imesababisha kushuka kwa Mrabaha na mapato mengine yanayokusanywa kutokana na madini hayo.

101.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali imeendelea kuongeza uwezo wa kusimamia madini yanayouzwa nje ya nchi kwa kudhibiti utoroshwaji wake. Udhibiti huo kwa Mwaka 2015 umewezesha kukamata na kutaifisha madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya Jumla ya **Dola za Marekani milioni 1.5** sawa na **Shilingi bilioni 3.34.** Madini hayo yalikamatwa katika matukio 25 kwenye viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere (Dar es Salaam) na KIA (Kilimanjaro).

102.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeongeza usimamizi katika eneo la Merelani kwa kuunda Kikosi Kazi cha kufuatilia uchimbaji na biashara ya Tanzanite. Kikosi Kazi hicho kimefanikisha: kukamatwa madini ya Tanzanite yenye uzito wa kilogramu 2.02 yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 1.21** sawa na **Shilingi bilioni 2.70** kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA); kukamata madini ya Tanzanite gramu 13,314.6 yenye thamani ya **Shilingi milioni 54.69** kutoka kwa wafanyabiashara wa ndani wasio na leseni; kuondolewa nchini kwa wafanyakazi 15 wa kutoka nje ya nchi waliokuwa wanafanya kazi katika Mgodi wa TanzaniteOne kinyume cha Sheria; na kujitokeza kwa Wafanyabiashara 361 kuomba leseni za udalali katika Ofisi za Arusha (194) na Merelani (167).

103.***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa biashara ya vito, Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Mineral Dealers Association (TAMIDA)* imeendesha Maonesho ya Kimataifa ya vito yaliyofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 19 hadi 21 Aprili, 2016. Katika Maonesho hayo madini yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.04** sawa na **Shilingi bilioni 9** yaliuzwa. Katika hatua za awali, Serikali ilikusanya Mrabaha wa **Dola za Marekani 158,597.46** sawa na **Shilingi milioni 353.34** na **Shilingi bilioni 1.36** zilipatikana kutokana na mauzo ya sehemu ya madini yaliyokamatwa yakitoroshwa nje ya nchi.

104.***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Serikali itaboresha usimamizi wa uzalishaji na biashara ya madini ili kuongeza mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa. Aidha, mpango mwingine ni kuendelea kuendesha minada ya ndani ya madini ya vito ikiwemo Tanzanite sambamba na kuimarisha udhibiti wa utoroshaji madini katika maeneo ya migodi na kwenye mipaka ya nchi.

**Malipo ya Ushuru wa Huduma**

105.***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015, Migodi ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi, North Mara, New Luika na Williamson Diamonds Limited imelipa ushuru wa huduma *(service levy)* wa Jumla ya **Shilingi bilioni 10.34** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 4.1** Mwaka 2014. Malipo hayo yameongezeka kwa **asilimia 152**. Ongezeko hili limechangiwa na Kampuni zenye *Mining Development Agreements (MDAs)* kulipa ushuru wa huduma wa **asilimia 0.3** ya mapato ghafi badala ya **Dola za Marekani 200,000** kwa Mwaka.

106.***Mheshimiwa Spika,*** mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo: Kampuni ya Acacia imelipa **Shilingi milioni 866.25** kwenye Halmashauri ya Kahama, **Shilingi bilioni 1.59** kwa Halmashauri ya Msalala na **Shilingi bilioni 2.01** kwa Halmashauri ya Tarime. Vilevile, Kampuni ya Shanta Gold Mining Limited imelipa **Shilingi milioni 831.41** kwa Halmashauri ya Chunya, Kampuni ya Williamson Diamonds Limited imelipa **Shilingi milioni 334.85** kwa Halmashauri ya Kishapu na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited imelipa **Shilingi bilioni 4.67** kwa Halmashauri ya Geita. Kampuni ya Almasi ya El-Hillal pia imelipa ushuru wa huduma wa **Shilingi milioni 27.57** Mwaka 2015 kwa Halmashauri ya Kishapu.

107.***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa wito kwa Viongozi wa Halmashauri husika **kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa na Kampuni za uchimbaji madini ikiwemo malipo ya ushuru wa huduma zinatumika katika shughuli za maendeleo kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla**.

**Kuendeleza Uchimbaji Mdogo wa Madini**

108.***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza **Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020, Ibara ya 35(m)(i) inayoelekeza kuwapatia maeneo Wachimbaji Wadogo,** kwa Mwaka 2015/16, Serikali ilitenga maeneo mawili (2) yenye ukubwa wa Hekta 7,731. Maeneo hayo yapo Nyamongo (Tarime) na Muhintiri (Singida) na yalipatikana kwa utaratibu wa ushirikiano kati ya Serikali na Kampuni za Acacia Mining Plc na Shanta Gold Mining Limited.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Serikali itatenga maeneo sita (6) yenye ukubwa wa takriban Hekta 12,000 kwa ajili ya uchimbaji

mdogo. Taratibu za kupatikana maeneo hayo zitazingatia taarifa za kijiolojia kutoka kwa Kampuni mbalimbali za utafutaji madini kwa kushirikisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST).

110. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza ahadi yake ya kuwapatia Ruzuku Wachimbaji Wadogo. Katika Mwaka 2015/16 Serikali imetoa Ruzuku ya **Shilingi bilioni 7.24** kwa Miradi 111 ya uchimbaji mdogo wa madini. Katika Mwaka 2016/17, **Dola za Marekani milioni tatu (3)** sawa na **Shilingi bilioni 6.68** zimetengwa kupitia Mradi wa SMMRP kwa ajili ya kutoa Ruzuku. Wizara itaendelea kutathmini maendeleo ya miradi iliyopata Ruzuku ili kuhakikisha inaleta manufaa.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kutenga maeneo kwa Wachimbaji Wadogo wa madini, Serikali ilitoa mafunzo kwa Wachimbaji Wadogo 181. Mafunzo hayo yalifanyika Mkoani Dodoma mwezi Oktoba, 2015 na yalihusu namna bora ya matumizi ya Ruzuku na utunzaji wa kumbukumbu. Aidha, mwezi Februari, 2016 Wafanyabiashara 23 wa madini walipewa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa utoaji taarifa za biashara ya madini. Mafunzo hayo yalifanyika Jijini Mwanza.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo mengine yalifanyika mwezi Machi, 2016 Jijini Dar es Salaam kwa viongozi 38 wa Vyama vya Wachimbaji Wadogo ambavyo ni FEMATA, TAWOMA, WIMA, TASPA na REMAS. Mafunzo hayo yalihusu mfumo wa utoaji wa taarifa za uchimbaji mdogo na kanzidata ya vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji madini. Katika Mwaka 2016/17, Wizara kupitia STAMICO na GST itaendelea kutoa huduma za ugani na mafunzo ya nadharia na vitendo kwa Wachimbaji Wadogo pamoja na Viongozi wa Wilaya na Halmashauri.

**Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini**

113. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2015/16 Wizara ilianzisha Mfumo wa malipo ya leseni kwa njia ya mtandao *(online payments system).* Mfumo huo ulianza rasmi tarehe 10 Desemba, 2015 kwa lengo la kuimarisha utoaji na usimamizi wa leseni za madini. Sambamba na hatua hiyo, Wizara imeendelea kusajili wateja zaidi kwenye Mfumo wa kupokea maombi ya leseni kwa njia ya mtandao *(Online Mining Cadastre Transactional Portal - OMCTP)*, hatua ambayo imeboresha utendaji na kupunguza mianya ya rushwa.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Jumla ya leseni 4,803 za utafutaji na uchimbaji wa madini zilisajiliwa kwenye Mfumo huo (OMCTP) kati ya leseni 38,695 zilizopo. Kati ya leseni hizo zilizosajiliwa: leseni 1,628 ni za utafutaji mkubwa wa madini; leseni 65 ni za uchimbaji mkubwa na wa kati; na leseni 3,110 ni za uchimbaji mdogo. Kwa upande wa umiliki wa leseni za utafutaji na uchimbaji mkubwa wa madini, Watanzania wanamiliki **asilimia 68** ya leseni zote, Wageni **asilimia 28** na **asilimia 4** ya leseni zinamilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na Wageni. Leseni za uchimbaji mdogo ambazo ni 35,273 zinamilikiwa kwa **asilimia 100** na Watanzania.

115. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kati ya mwezi Julai, 2015 na Machi, 2016 Jumla ya maombi ya leseni 8,025 ya utafutaji na uchimbaji madini yalipokelewa. Jumla ya leseni 4,782 zilitolewa ambapo kati ya hizo, leseni 112 ni za utafutaji mkubwa wa madini, leseni 12 za uchimbaji wa kati, leseni moja (1) ya uchimbaji mkubwa na leseni 4,657 ni za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, maombi 2,716 ya leseni yalikataliwa kwa kushindwa kukidhi masharti. Maombi 527 yanaendelea kuchambuliwa kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

116. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kufanya ukaguzi wa maeneo ya leseni na uchambuzi wa taarifa za utendaji kwenye leseni za madini. Uchambuzi wa taarifa za leseni umewezesha kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya leseni zao. Hatua za kisheria zimeendelea kuchukuliwa kwa wamiliki wasiotimiza masharti ya leseni.

117. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kati ya mwezi Julai, 2015 na Machi, 2016, Jumla ya leseni 1,330 zilifutwa. Kati ya leseni hizo, 151 zilikuwa ni za utafutaji madini na 1,179 ni za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, hati za makosa *(default notice)* 117 zilitolewa kwa leseni 111 za utafutaji madini na 6 za uchimbaji wa kati. **Napenda kutoa wito kwa wamiliki wa leseni za madini kutimiza masharti yaliyowekwa kwenye leseni hizo ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufuta leseni zao**.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuboresha huduma kwa wateja ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za leseni za madini kwa njia ya Mtandao. Aidha, usimamizi wa leseni utaimarishwa ili kuhakikisha kuwa wamiliki wote wa leseni wanatimiza masharti ya kisheria. Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko na migogoro katika Sekta ya Madini kwa

kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali, zikiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

119. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha utunzaji wa taarifa na takwimu katika Sekta ya Madini. **Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imejenga na kuanzisha Kituo Maalum cha Kuhifadhi Takwimu za Madini *(Data Recovery Centre)***. Kituo hicho ambacho kimejengwa Mjini Morogoro kilianza kazi rasmi mwezi Februari, 2016. Kituo hicho kitawezesha Serikali kuwa na uhakika wa upatikanaji wa taarifa zinazohusu Sekta ya Madini kwa nchi nzima endapo litatokea tatizo katika Ofisi yoyote ya Madini huko Mikoani.

**Kuimarisha Usimamizi wa Masuala ya Baruti Nchini**

120. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za uagizaji, uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi na matumizi ya Baruti ziliendelea. Jumla ya tani 22,229 za Baruti ziliingizwa nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikilinganishwa na tani 24,308 za Baruti zilizoingizwa Mwaka 2014/15 sawa na upungufu wa **asilimia 9**. Upungufu huo unatokana na shughuli za utafiti wa madini kupungua kwa kipindi husika kwa sababu ya kushuka kwa bei za madini, hususan dhahabu, shaba na fedha kwenye Soko la Dunia.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia iliendelea kusimamia uingizaji wa fataki ambapo kwa kipindi cha kati ya mwezi Julai, 2015 na Januari, 2016 vipande 4,189,337 viliagizwa. Fataki hizo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo uchimbaji madini, utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na miradi ya ujenzi wa miundombinu. Aidha, Wizara ilitoa vibali 86 vya kuingiza Baruti nchini, vibali 75 vya kulipulia Baruti na leseni 9 za maghala ya kuhifadhia Baruti.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa masuala ya Baruti nchini. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu na mafunzo ya matumizi bora na salama ya Baruti kwa Wachimbaji Wadogo na wadau wengine wa Baruti ambao wanafikia takriban 800 nchi nzima.

**Usimamizi wa Migodi Nchini**

123. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2015/16, Jumla ya Migodi 1,241 ilifanyiwa ukaguzi wa masuala ya afya, usalama na utunzaji wa mazingira. Ukaguzi huo ulifanyika katika Migodi Mikubwa minne ya dhahabu ambayo ni North Mara, Bulyanhulu, Buzwagi, Geita

na Mgodi wa almasi wa Mwadui; Migodi ya Kati 75; na Migodi Midogo 1,161. Ukaguzi huo ulilenga kuboresha afya, usalama na utunzaji mazingira migodini kwa kuzingatia Taratibu na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha uwezo wa Wakaguzi wa Migodi, mwezi Novemba, 2015 Wizara iliendesha mafunzo yanayohusu usalama katika Migodi ya Makaa ya Mawe. Mafunzo hayo yalifanyika Mjini Bagamoyo Mkoa wa Pwani na yalihusisha Wakaguzi 75. Mafunzo hayo yalitolewa na Wakufunzi wa *Centre for Science and Environment* kutoka nchini India. Aidha, Wizara imeanzisha Timu ya Uokoaji (*Mine Rescue Team*) itakayofanya kazi ya uokoaji katika matukio ya ajali yanayotokea migodini. Timu hiyo iliyoundwa mwezi Oktoba, 2015 ina Wakaguzi wa Migodi 17 kutoka Ofisi za Madini na imeanza kupatiwa mafunzo kuhusu masuala ya uokoaji.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kusimamia na kuboresha afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini, katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa migodi ya Wachimbaji Wadogo, wa kati na wakubwa na imepanga kufanya ukaguzi kwa Jumla ya Migodi 1,500 nchini. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Utunzaji Mazingira *(Environmental Protection Plan - EPP)* kwa Wachimbaji Wadogo wa madini. Pia, Wizara itakamilisha Mikataba kati yake na migodi inayomilikiwa na Kampuni ya Acacia (Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara) kwa ajili ya kuweka Hati Fungani *(rehabilitation bond)* ifikapo Mwezi Juni, 2016.

**Kuimarisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini Nchini**

126. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini ambapo Jumla ya Leseni 20 za uchenjuaji madini ya dhahabu zilitolewa na kufikia Jumla ya Leseni 162. Kutolewa kwa leseni hizo kumeongeza chachu ya wananchi kuendelea kushiriki zaidi katika shughuli za kuongeza thamani madini, hususan uchenjuaji wa marudio ya dhahabu. Aidha, ongezeko la leseni hizo limewezesha Serikali kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za uchenjuaji dhahabu. Katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 **Shilingi bilioni 2.9** zilikusanywa ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 2.2** zilizopatikana kipindi kama hicho katika Mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la **asilimia 32**.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuhamasisha na kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini. Kipaumbele kitawekwa katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda ili kuwezesha Watanzania wengi kushiriki katika shughuli hizo.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Jemolojia Tanzania *(Tanzania Gemological Centre – TGC)* cha Arusha kiliandaa mitaala ya kufundishia fani za *gemology*, *jewelry design & manufacturing* na *stone carving*. Aidha, taratibu za kukisajili Kituo hicho NACTE zinaendelea. Katika Mwaka 2015/16, Kituo kimetoa mafunzo ya kukata na kusanifu madini ya vito kwa Wanawake 14 na hivyo kuongeza idadi ya wahitimu wa mafunzo hayo kufikia Wanawake 29.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kimeendelea kujiimarisha kwa kununua vifaa vya kufundishia mafunzo ya Jemolojia vikiwemo *gemological microscopes 25, refractometer 25, spectroscope* 25, *diamond tester 10, digital refractometer* na *hydrostatic balance*. Vifaa vingine vilivyonunuliwa ni kwa ajili ya kufundishia usanifu na usonara ambavyo ni pamoja na *computer* 8, *GEMCAD software* 5, 3-D *wax printer* 3, *card printer* 3, *wire wrapping*, *forming*, *soldering* na *cutting tools*. Vilevile, mashine 21 za kukata na kung'arisha madini ya vito (*faceting machines*) zilinunuliwa. Jumla ya **Dola za Marekani milioni 1.3** sawa na takriban **Shilingi bilioni 2.9** zimetumika katika ununuzi wa vifaa hivyo kupitia Mkopo kutoka Benki ya Dunia chini ya Mradi wa SMMRP.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Kituo kitaanzisha maabara ya utambuzi wa madini ya vito pamoja na kutoa vyeti vya uthibitisho *(Certificate of Authenticity*). Aidha, shughuli za utafiti *(research and design)*, huduma za ushauri na ugani zitatolewa kwenye madini ya vito na usonara. Vilevile, huduma nyingine itakayotolewa ni ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito kwa Wajasiriamali na Wachimbaji Wadogo.

**Uchambuzi na Uthaminishaji wa Madini ya Vito**

131. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2015/16, Wizara iliendelea na usimamizi wa tasnia ya almasi na vito. Katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Februari, 2016 karati 129,329 za almasi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 40.90** zilithaminishwa. Kutokana na mauzo hayo, Serikali ilipata Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 2.04** sawa na **Shilingi bilioni 4.42**.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** madini ya vito yalithaminishwa kama ifuatavyo: tani 1,299.48 za madini ya mapambo, gramu milioni 2.02 za vito ghafi na karati 66,849.24 za madini ya vito yaliyochongwa. Madini hayo yalithaminishwa kwa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 15.32** na yaliipatia Serikali Mrabaha wa **Dola za Marekani 608,580.79** sawa na **Shilingi bilioni 1.36**. Katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuimarisha shughuli za uchambuzi na uthaminishaji wa madini ya almasi na vito ili kuongeza mapato kwa Serikali.

**Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(SMMRP)***

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa *SMMRP* upo katika awamu ya pili ya utekelezaji ambayo ilianza rasmi Septemba, 2015 na itaisha Desemba, 2018. Katika Mwaka 2015/16, Mradi umewezesha ukarabati wa Ofisi za Madini za Mtwara, Moshi, Nachingwea na Tunduru. Aidha, ununuzi wa vifaa vya mafunzo kwa ajili ya Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na vitendea kazi kwa Ofisi za Madini za Bariadi, Moshi, Nachingwea, Njombe na Songea umefanyika. Fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na ukarabati wa Ofisi hizo ni **Shilingi bilioni 1.35** ambazo zimetolewa na Benki ya Dunia.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, kupitia Mradi wa *SMMRP* kazi zifuatazo zitatekelezwa: ukarabati na upanuzi wa Ofisi za Madini za Bariadi, Bukoba, Chunya, Kigoma, Mpanda, Musoma na Songea; Ofisi za STAMICO (Dar es Salaam) na Chuo cha Madini (Dodoma). Kupitia Mradi huu, vifaa mbalimbali vya ugani vitanunuliwa ili kusaidia Wachimbaji Wadogo wa madini kupitia STAMICO, GST na Ofisi za Madini za Kanda. Aidha, Mradi utawezesha GST kufanya utafiti katika maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za uchimbaji mdogo na yale yanayopendekezwa kuwa vituo vya mafunzo. Lengo ni kutathmini mashapo yaliyopo na hivyo kuwawezesha Wachimbaji Wadogo kufanya shughuli zao kwa uhakika zaidi.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itaanzisha Vituo saba (7) vya mfano vya kuchenjua madini kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo katika Mikoa ya Kagera, Katavi, Lindi, Mara, Mbeya, Ruvuma na Shinyanga. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuendeleza Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na kuwezesha usimikaji wa Mtandao wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Ofisi za Madini za Bariadi, Mbeya, Moshi, Mtwara, Nachingwea na Njombe. Makadirio ya ujenzi wa vituo hivyo ni **Dola za Marekani milioni 6** sawa na **Shilingi bilioni 13.4**.

**Miradi Mikubwa ya Madini**

136 ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na bei ya madini ya dhahabu na nikeli kushuka katika Soko la Dunia, Serikali imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa miradi mikubwa ya madini. Uhamasishaji huo unahusisha pia madini ya *graphite* ambayo bei zake hazijaathirika katika Soko la Dunia. Miongoni mwa miradi ya madini ambayo ipo katika hatua za uendelezaji ni pamoja na Mradi wa *graphite* uliopo Nachu Wilaya ya Ruangwa na Mradi wa *graphite* uliopo Epanko Wilaya ya Ulanga.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi mingine iliyopo katika hatua za uendelezaji ni Mradi wa Urani uliopo eneo la Mto Mkuju Wilaya ya Namtumbo na Mradi wa Niobium uliopo Wilaya ya Songwe. Madini ya Niobium hutumika katika utengenezaji wa vifaa vya kieletroniki. Upembuzi yakinifu wa Miradi hii miwili umekamilika.

**Utatuzi wa Migogoro katika Uchimbaji Madini**

138. ***Mheshimiwa Spika,*** kero na migogoro mbalimbali ya madini imeendelea kutatuliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inaendeshwa kwa amani. Mojawapo ya mgogoro ni leseni 15 za utafutaji madini ya dhahabu zilizotolewa karibu na eneo la Kambi ya Jeshi lililopo Kiabakari, Wilaya ya Butiama. Aidha, kuna maombi mengine ya leseni za utafiti ambayo yamo ndani ya eneo la Kambi hii. Katika utatuzi wa mgogoro huu, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kutafuta ufumbuzi wa suala hilo.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** upo mgogoro unaohusu eneo la Nyarugusu, hususan Kitongoji cha Buziba, Mkoa wa Geita ambalo wananchi wamekuwa wakiliomba kwa muda mrefu ili kuchimba madini ya dhahabu. Eneo hilo lina leseni hai ya utafiti wa madini inayomilikiwa kwa ubia kati ya STAMICO na Kampuni ya Mineral Royalty ya Canada. Pamoja na kuwepo kwa leseni hiyo, Serikali inakamilisha taratibu za kisheria za kuchukua sehemu ya eneo hilo kwa ajili ya kuligawa kwa wananchi. Katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kutatua migogoro iliyopo katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji madini nchini.

**Sheria katika Sekta ya Madini**

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Rasimu za Sheria za Baruti na Uongezaji Thamani Madini zimekamilika. Lengo la Sheria hizo ni kuimarisha usimamizi

katika matumizi ya Baruti na Fataki pamoja na shughuli za uongezaji thamani madini. Hata hivyo, Wizara inaendelea kukusanya maoni zaidi kutoka kwa wadau muhimu ili kuziboresha Rasimu hizo. Katika Mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha Rasimu hizo na kuziwasilisha katika Mamlaka husika ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ajili ya maamuzi.

**Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST)**

141. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala ulikusanya taarifa zitakazowezesha kuchorwa kwa Ramani kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji *(Mineral Promotion Block Map)* katika Wilaya za Masasi, Nachingwea na Tunduru. Wakala pia kwa kushirikiana na *Geological Survey of Finland* (GTK) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) unaendelea na kazi ya uchunguzi wa maabara wa sampuli za udongo zilizokusanywa katika Wilaya hizo. Matokeo ya uchunguzi wa udongo yatawezesha Wakala kuchora Ramani za Jiokemia *(Multi-Element Geochemical Atlas)* kwa Wilaya hizo tatu.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Wakala utachapisha Ramani kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji katika Wilaya hizo na taarifa zake baada ya kupata matokeo ya utafiti kutoka maabara. Kazi hizo zinagharimu Jumla ya **Euro 700,000** sawa na takriban **Shilingi bilioni 1.74** na zinafadhiliwa na Serikali ya Finland.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha Wachimbaji Wadogo, Wakala ulifanya utafiti wa kina wa Jiokemia na Jiofizikia katika maeneo ya Kyerwa Mkoa wa Kagera. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kubaini kiasi na mwelekeo wa mbale ya madini *(ore)* ya bati *(tin)*. Matokeo ya utafiti yatasaidia Wachimbaji Wadogo kuchimba kwa kufuata mwelekeo wa mbale na hivyo kuwa na uchimbaji salama na wenye tija kwa lengo la kuongeza kipato chao. Kazi ya utafiti itakamilika Mwezi Juni, 2018 na itagharimu **Shilingi milioni 640** na fedha hizo zitatoka Mradi wa SMMRP.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, GST itafanya utafiti wa jiokemia, jiolojia, jiofizikia na tabia za mbale *(ore characteristics)* katika maeneo ya Endabash (Manyara), Handeni (Tanga), Ibindi (Katavi), Itumbi (Mbeya), Kapanda (Katavi), Katente (Geita), Kilindi (Tanga), Kyerwa (Kagera), Merelani (Manyara), Mgusu (Geita), Mvomero (Morogoro),

Nyamongo (Mara) na maeneo ya Mkoa wa Singida ya Kilondata, Londoni Sambaru, Mpambaa na Muhintiri. Lengo ni kusaidia Wachimbaji Wadogo namna ya kutafuta mwelekeo wa mbale pamoja na kuwaelimisha kuhusu uchimbaji na uchenjuaji salama na wenye tija.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile GST itafanya kazi maalum *(field checks)* ya jiolojia na jiokemia ili kuboresha Ramani za QDS 49, 64 na 65. Kazi hiyo itasaidia kukusanya na kuhakiki taarifa za uwepo wa madini nchini na kuboresha kanzidata yake. Wakala utaendelea kuratibu majanga ya asili ya jiolojia ikiwa ni pamoja na matetemeko ya ardhi na milipuko ya volkeno. Wakala pia utabaini maeneo yenye hatari ya kupata maporomoko ya ardhi ikiwemo Safu za Milima ya Usambara na kutoa ushauri kwa wananchi waishio katika maeneo hayo.

**Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA)**

146. ***Mheshimiwa Spika***, TMAA imeendelea na kazi ya ukaguzi wa Hesabu za Fedha za Migodi na kuwezesha Kodi ya Mapato ya Jumla ya **Shilingi bilioni 107.7** kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Fedha hizo zimekusanywa kutoka Kampuni za Geita Gold Mining Limited (**Shilingi bilioni 76.03**), North Mara Gold Mining Limited (**Shilingi bilioni 31.2**) na Resolute Tanzania Limited (**Shilingi milioni 472**) katika kipindi kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016. Pia, ukaguzi huo umewezesha Serikali kukusanya Kodi na Tozo nyingine zenye Jumla ya **Shilingi bilioni 2.79** kutoka Migodi Mikubwa na ya Kati iliyokaguliwa katika kipindi hicho.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** ukaguzi uliofanywa na Wakala kwa kushirikiana na Ofisi za Madini za Kanda umewezesha Serikali kukusanya Mrabaha wa **Shilingi bilioni 5.1** kutokana na shughuli za uzalishaji na biashara ya madini ya ujenzi na viwandani. Fedha hizo zilizokusanywa katika kipindi kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 ni ongezeko la **asilimia 16** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 4.4** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka 2014/15.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 Wakala ulifanya ukaguzi na uhakiki wa madini katika Migodi Mikubwa na ya Kati. Ukaguzi huo uliwezesha mrabaha wa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 52** sawa na takribani **Shilingi bilioni 115.85** kulipwa Serikalini. Malipo hayo yalikuwa kama ifuatavyo: Bulyanhulu **Dola za Marekani milioni 10.53**; Buzwagi **Dola za Marekani milioni 5.88**; Geita **Dola za Marekani milioni 17.88**; North Mara **Dola za Marekani milioni**

**9.95**; Mwadui **Dola za Marekani milioni 3.37**; New Luika **Dola za Marekani milioni 3.36**; STAMIGOLD Biharamulo **Dola za Marekani milioni 0.75**; TanzaniteOne **Dola za Marekani milioni 0.05**; na Ngaka **Dola za Marekani milioni 0.25**.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini katika migodi kupitia TMAA. Lengo ni kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali ya madini na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa.

**Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

150. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 STAMICO kupitia Kampuni yake Tanzu ya STAMIGOLD imezalisha na kuuza wakia 17,346 za dhahabu. Madini hayo yalikuwa na thamani ya **Dola za Marekani milioni 19.80,** sawa na takriban **Shilingi bilioni 44.11**. STAMICO ilipata **Shilingi milioni 426.49** kutoka STAMIGOLD ikiwa ni ada ya usimamizi *(management fee)*.

151. ***Mheshimiwa Spika***, kati ya Mwezi Julai, 2015 na Machi, 2016 Mgodi wa TanzaniteOne unaomilikiwa kwa ubia wa asilimia 50 kwa 50 kati ya STAMICO na Kampuni ya Sky Associates ulizalisha karati 10,927,080 za Tanzanite. Madini hayo ya Tanzanite yalikuwa na thamani ya **Dola za Marekani milioni 1.4**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 3.12**. STAMICO imepata **Shilingi milioni 30.43** kutoka TanzaniteOne ikiwa ni ada ya usimamizi.

152. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika limekamilisha utafiti wa awali wa kijiolojia katika leseni yake ya madini adimu (*Rare Earth Elements)* iliyopo eneo la Sengeri Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe. Matokeo ya utafiti huo wa awali yameonesha uwepo wa madini hayo ambayo hutumika kutengeneza vifaa vya kisasa vya kielektroniki. Shirika pia limekamilisha utafiti wa awali wa madini ya chuma *(iron ore)* na *feldspar* katika leseni yake iliyopo Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro ambapo matokeo ya maabara yameonesha uwepo wa madini ya chuma katika eneo hilo.

153. ***Mheshimiwa Spika***, STAMICO imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wachimbaji Wadogo ili kuboresha shughuli zao za uchimbaji. Mwezi Februari, 2016 Shirika lilikamilisha na kuzindua tovuti ya uchimbaji mdogo *(Small Scale Mining Portal)*. Jumla ya Wachimbaji Wadogo na

Wafanyabiashara wa madini 35 walipatiwa mafunzo ya jinsi ya kuunganishwa na kutumia tovuti hiyo.

154. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani limefanikiwa kununua mashine ya uchorongaji *(Drilling Rig)* moja yenye thamani ya **Dola za Marekani 350,000** sawa na takriban **Shilingi milioni 780.** Kununuliwa kwa mashine hiyo kutaongeza uwezo katika kazi za uchorongaji na utafiti kwenye maeneo yanayomilikiwa na Shirika, Wachimbaji Wadogo na kukodisha kwa wadau wengine wanaohitaji huduma hiyo.

155. ***Mheshimiwa Spika***, STAMICO ilifanya uchambuzi yakinifu kuona uwezekano wa kujenga kiwanda cha kuchenjua mabaki ya dhahabu katika Mgodi wa Buhemba. Ilibainika kuwa, katika mabaki ya mchanga wa dhahabu ambayo ni tani 796,400 kuna dhahabu gramu 1.07 kwa kila tani ambazo kwa mabaki yote ya dhahabu wastani wa kilo 682 za dhahabu zitapatikana (ikichukuliwa kuwa asilimia 80 ya mabaki ya mchanga utakaochenjuliwa yatatoa dhahabu). Katika Mwaka 2016/17, **Shilingi bilioni 10.58** kutoka vyanzo vya ndani vya STAMICO zitatumika kununua mashine ya kuchenjua mabaki ya dhahabu.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imetekeleza kazi mbalimbali za kuendeleza Mradi wa kuzalisha umeme wa MW 200 wa Makaa ya Mawe wa Kiwira, Mbeya zikiwemo: kukamilisha tathmini ya awali ya maeneo yatakayoathiriwa na njia ya kupitisha umeme yenye urefu wa kilomita 100 kutoka Kiwira hadi Mwakibete Jijini Mbeya; kupitia upya taarifa za mashimo ya kijiolojia *(drill hole data)* kwa ajili ya kutathmini kiasi cha mashapo ya makaa ya mawe kilichopo kwenye leseni za Ivogo na Kabulo; na kuandaa *Concept Note* ya Mradi kwa ajili ya kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

157. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2016/17, STAMICO itaendelea kufufua Mradi wa Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira kwa nia ya kuzalisha umeme wa MW 200, ambapo **Shilingi bilioni 2** zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu.

**Chuo cha Madini - MRI**

158. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua za kukipandisha hadhi Chuo cha Madini Dodoma ziliendelea ambapo mwezi Desemba, 2015 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) lilikipa mamlaka kamili ya kujitegemea kitaaluma na kiutawala *(Autonomous Status).* Chuo hicho kilipata idhini

ya kuwa *Dodoma Polytechnic of Energy and Earth Resources Management*. Kutokana na hadhi hiyo, Chuo hicho kitajiendesha kwa kufuata taratibu za NACTE na kuboresha taaluma zinazotolewa. Kwa sasa taratibu za mwisho za kufikia hadhi hiyo zinaendelea ikiwemo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya elimu kuwasilisha Bungeni tamko husika kabla ya mwisho wa Mwaka 2016.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo pia kimekamilisha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 88 kwa wakati mmoja. Vilevile, Chuo kimekamilisha ukarabati na upanuzi wa Jengo la Bwalo la chakula na sasa lina uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 kwa pamoja tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo uwezo wake ulikuwa wanafunzi 50. Aidha, katika Mwaka 2015/16 Chuo kimedahili wanafunzi 586 katika fani mbalimbali. Jumla ya wanafunzi 182 wanatarajiwa kuhitimu mwezi Mei, 2016 katika ngazi ya stashahada ambapo kati yao wanawake ni 14 na wanaume ni 168. Wizara ya Nishati na Madini imetoa ufadhili wa **Shilingi milioni 539.34** kwa wanafunzi 178 waliojiunga katika fani za Mafuta na Gesi Asilia. Katika Mwaka 2016/17, Chuo kitaendelea kuimarisha utendaji wake kwa kuandaa fani mpya za masomo na kuendeleza watumishi na miundombinu.

**Asasi ya Uwazi katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative – TEITI)***

160. ***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyoahidiwa na Serikali, Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania *(Tanzania Extractive Industries Transparency and Accountability Act, 2015)* ilipitishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 455 la tarehe 16 Oktoba, 2015. Pamoja na mambo mengine, lengo la Sheria hiyo ni kuipa nguvu ya kisheria Kamati ya TEITI ya kuzitaka Kampuni kuweka wazi taarifa za malipo, mauzo na gharama za uwekezaji; na Serikali kutakiwa kuweka wazi taarifa zake za mapato yanayotokana na rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na matumizi ya mapato hayo.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha maandalizi ya Kanuni za Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania ya Mwaka 2015. Aidha, Rejista ya Majina ya Wamiliki Hisa kwenye Leseni na Mikataba katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia itaanzishwa ili kuwatambua kwa majina wanaomiliki Hisa katika Kampuni Binafsi.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba, 2015 Kamati ya TEITI ilikamilisha na kutoa kwa umma taarifa za ulinganisho kwa Mwaka 2012/13 na 2013/14. Taarifa ni za malipo ya kodi yaliyofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa Serikali Kuu na katika Halmashauri ambazo zinapokea Tozo kwa mujibu wa Sheria. Taarifa hizo zilibainisha baadhi ya Kampuni kubwa za uchimbaji wa madini ya dhahabu na vito ambazo hazijaanza kulipa Kodi ya Mapato *(Corporate Tax)*. Kampuni hizo ni Acacia Mining (inayomiliki Migodi ya Bulyanhulu, North Mara na Buzwagi), Shanta Mining na TanzaniteOne Mining Limited.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa hizo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzielekeza Kampuni hizo kulipa Kodi ya Mapato na malimbikizo yote. Kufuatia hatua hizo, Kampuni ya Acacia imelipa Kodi ya Mapato ya **Dola za Marekani milioni 14** sawa na takriban **Shilingi bilioni 31.2** kwa Mgodi wake wa North Mara Mwezi Machi, 2016.

**AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU**

164. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza tija na motisha kwa watumishi, kwa Mwaka 2015/16 Wizara iliwapandisha vyeo Jumla ya watumishi 38 katika fani mbalimbali, kuwathibitisha kazini watumishi 108 na kuwabadilisha watumishi 11 kutoka kwenye kada moja kwenda nyingine *(re-categorization)*.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuajiri na kuendeleza watumishi wake ili waweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi. Katika Mwaka 2015/16, Jumla ya watumishi walioajiriwa na Wizara na Taasisi zake katika kada mbalimbali ni 179. Kati ya hao, Wizara iliajiri watumishi 68, TMAA 22, REA 6, TPDC 36, GST 44 na STAMICO 3.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kutoa ufadhili wa masomo kwa Watanzania katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia. Mafunzo hayo hutolewa katika shahada za uzamili na uzamivu ili kuiwezesha nchi kuwa na Wataalamu wa Kitanzania katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia. Katika Mwaka 2015/16, Watanzania 18 walipata ufadhili wa mafunzo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kupitia *Energy Sector Capacity Building Program* inayoratibiwa na Wizara, Jumla ya Watanzania 321 walipata ufadhili wa mafunzo ambapo kati ya hao, 112 walihudhuria mafunzo ya

muda mfupi; 178 stashahada; na 31 walihudhuria mafunzo ya shahada za uzamili katika fani mbambali zikiwemo za Mafuta na Gesi Asilia. Fedha zilizotumika kwa ajili ya mafunzo hayo ni **Dola za Marekani 506,000** sawa na **Shilingi bilioni 1.13**. Fedha hizo zimetolewa kupitia Mkopo wa Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Canada (CIDA). Katika Mwaka 2016/17 Serikali itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwapatia lishe na madawa maalumu watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) na wenye UKIMWI kulingana na miongozo iliyopo. Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kujiepusha na tabia ambazo zinaweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI na kupima afya zao mara kwa mara. Katika kipindi cha kati ya Julai, 2015 na Machi, 2016 Jumla ya **Shilingi milioni 12.6** zimetolewa kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

## USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

169. ***Mheshimiwa Spika,*** Washirika wa Maendeleo wameendelea kushirikiana na Wizara katika shughuli mbalimbali, hususan kwenye miradi ya maendeleo na kuwajengea watumishi uwezo. Kwa kutambua mchango huo, na kwa niaba ya Serikali natumia fursa hii kutoa shukurani kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya BADEA, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Exim ya China, Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC) na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Vilevile, natoa shukurani kwa Taasisi na Mashirika ya AFD (Ufaransa), CIDA (Canada), ECDF (Korea Kusini), ICEIDA (Iceland), FINIDA (Finland), JICA (Japan), KfW (German), NORAD (Norway), OFID (Saudi Arabia), ORIO (Uholanzi), Sida (Sweden), UNDP, USAID (Marekani) na Umoja wa Ulaya (EU).

## B. SHUKURANI

170. ***Mheshimiwa Spika,*** natumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mbunge wa Jimbo la Chato, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini. Natambua uzoefu wake katika Sekta za Nishati na Madini na ninamshukuru kwa dhati kwa jinsi anavyoshirikiana nami katika kusimamia Wizara hii. Natoa shukurani pia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Prof. Justin William Ntalikwa, pamoja na Naibu Makatibu Wakuu Prof. James

Epifani Mdoe na Dkt. Juliana Leonard Pallangyo kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa katika kusimamia majukumu ya Wizara.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** ufanisi wa Sekta za Nishati na Madini kwa kiasi kikubwa unategemea Wataalam wa fani mbalimbali. Hivyo, natumia fursa hii kuwashukuru watumishi wa Wizara wakiongozwa na Kamishna wa Nishati na Masuala ya Petroli; Kamishna wa Madini; na Wakuu wa Idara na Vitengo kwa kutekeleza majukumu yao ya kazi ipasavyo. Vilevile, nawashukuru Wenyeviti wa Bodi pamoja na Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mzuri wanaonipa.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Wananchi wa Tanzania kwa ujumla kwa kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ikiwemo kunipatia taarifa muhimu katika Sekta ninazosimamia. Aidha, natoa shukurani kwa wananchi wa Jimbo langu la Musoma Vijijini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na imani waliyonayo kwangu katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu. Kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa kunitia moyo na kunifariji katika kutekeleza majukumu yangu.

## C. HITIMISHO

173 ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2016/17 ni Jumla ya **Shilingi 1,122,583,517,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,056,354,669,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 94**. Kwa kuzingatia ***Ibara ya 43(a) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020*** inayoelekeza Serikali kuongeza kiwango kikubwa cha uzalishaji wa nishati ili kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa, **asilimia 98** ya Bajeti ya Maendeleo imetengwa kwa ajili ya Sekta ya Nishati.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 66,228,848,000** sawa na **asilimia 6** ya Bajeti yote. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 38,871,230,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* sawa na **asilimia 59** na **Shilingi 27,357,618,000** sawa na **asilimia 41** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja.

# *VIELELEZO VYA HOTUBA YA MWAKA 2016/17 KUHUSU SEKTA ZA NISHATI NA MADINI*

## A. SEKTA YA NISHATI


***Kielelezo Na. 1: Bei Mpya za Umeme Zilizoidhinishwa na EWURA kuanzia Mwezi Aprili, 2016***

| Kundi la Mteja | Aina ya Bei/ Tozo | Uniti | Bei za Awali | Bei Zilizoidhinishwa 2016 | % Mabadiliko |
|---|---|---|---|---|---|
| D1 | Bei ya Nishati (0 - 75 kWz) | TZS/kWh | 100 | 100 | 0.0% |
| | Bei ya Nishati (Zaidi ya 75 Kwh) | TZS/kWh | 350 | 350 | 0.0% |
| T1 | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | 5,520 | - | -100.0% |
| | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 298 | 292 | -2.0% |
| T2 | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | 14,233 | 14,233 | - |
| | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 200 | 195 | -2.3% |
| | Bei ya Mahitaji ya Juu | TZS/kVA/ Mwezi | 15,004 | 15,004 | |
| T3-MV | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | 16,769 | 16,769 | - |
| | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 159 | 157 | -1.5% |
| | Bei ya Mahitaji ya Juu | TZS/kVA/ Mwezi | 13,200 | 13,200 | |
| T3-HV | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 156 | 152 | -2.4% |
| | Bei ya Mahitaji ya Juu | TZS/kVA/ Mwezi | 16,550 | 16,550 | - |

| **Kielelezo** |
|---|
| D1: Wateja wa majumbani ambao wana matumizi madogo ya wastani wa uniti 75 kwa mwezi. Matumizi yatakayozidi uniti 75 yatatozwa bei ya juu ya Shilingi 350 kwa kila uniti moja inayozidi. Kwa Kundi hili la wateja, umeme unatolewa katika Msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V). |
| T1: Wateja wenye matumizi ya kawaida hususani wateja wa majumbani, kwenye biashara ndogondogo, viwanda vidogo, taa za barabarani, mabango n.k. Umeme unatolewa katika Msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V) na njia tatu (400V). |
| T2: Wateja wenye matumizi ya kawaida ya umeme kupitia 400V na matumizi kwa mwezi ni zaidi ya uniti 7,500. |
| T3-MV: Wateja walioounganishwa katika Msongo wa kati wa umeme (Medium Voltage). |
| T3-HV: Wateja walioounganishwa katika Msongo mkubwa wa umeme (High Voltage) ikijumuisha ZECO, Bulyanhulu na Twiga Cement. |


*Chanzo: EWURA- Aprili, 2016*

***Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Uagizaji Mafuta Nchini kwa ajili ya Matumizi ya Ndani ya Nchi (Januari hadi Desemba, 2015)***




*Chanzo: PBPA- Aprili, 2016*

***Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Uagizaji Mafuta Nchini kwa ajili ya Nchi Jirani (Januari hadi Desemba, 2015)***




*Chanzo: PBPA- Aprili, 2016*


***Kielelezo Na. 4: Kiasi cha Gesi Asilia Kilichogunduliwa Nchini hadi Aprili, 2016***

| **Kitalu cha Ugunduzi** | **Visima vya Uzalishaji/ Ugunduzi** | **Mwaka ilipogun-dulika** | **Msimamizi *(Operator)*** | **Hatua Iliyofikiwa** | **Kiasi cha Gesi Kilichogunduliwa (TCF)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Songosongo | S4, S7,S10 & S11 | 1974 | Panafrican Energy | Imeendelezwa | 1 – 2.5 |
| Mnazi-bay | MB1,MB2,MB3&MS-x1 | 1982 | M &P | Imeendelezwa | 3 – 5 |
| Mkuranga | Mkuranga-1 | 2007 | M&P | Haijaendelezwa | 0.2 |
| Nyuni | Kiliwani-N | 2008 | Ndovu Resource | Haijaendelezwa | 0.07 |
| Ruvuma | Ntorya-1 | 2012 | Ndovu Resource | Haijaendelezwa | 0.178 |
| Ruvu | Mambakofi-1 | 2015 | Dodsal | Haijaendelezwa | 2.17 |
| **JUMLA YA KIASI CHA GESI ASILIA KILICHOGUNDULIWA NCHI KAVU** | | | | | **4.45 - 10.118** |
| Block 1 | Chaza-1 | 2011 | BG Tz | Haijaendelezwa | 0.47 |
| | Jodari-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | 3.53 |
| | Jodari North-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | |
| | Jodari South-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | |
| | Mzia-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | 8.5 |
| | MZIA-2 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | |
| | Mzia- 3 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | |
| | Mkizi -1 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | 0.6 |
| | Taachui-1 | 2014 | BG Tz | Haijaendelezwa | 1.10 |
| Block 2 | Zafarani-1 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | 6.0 |

| Kitalu cha Ugunduzi | Visima vya Uzalishaji/ Ugunduzi | Mwaka ilipogun-dulika | Msimamizi *(Operator)* | Hatua Iliyofikiwa | Kiasi cha Gesi Kilichogunduliwa (TCF) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Zafarani-2 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | |
| | Lavani-1 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | 3.6 |
| | Lavani-2 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | 1.4 |
| | Tangawizi-1 | 2013 | Statoil | Haijaendelezwa | 5.4 |
| | Mronge -1 | 2013 | Statoil | Haijaendelezwa | 2.5 |
| | Piri-1 | 2014 | Statoil | Haijaendelezwa | 3.0 |
| | Giligiliani-1 | Aug-14 | Statoil | Haijaendelezwa | 1.7 |
| | Mdalasini | Mar-15 | Statoil | Haijaendelezwa | 1.8 |
| Block 3 | Papa-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | 2.0 |
| Block 4 | Chewa-1 | 2010 | BG Tz | Haijaendelezwa | 1.8 |
| | Pweza-1 | 2010 | BG Tz | Haijaendelezwa | 1.9 |
| | Ngisi - 1 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | 0.8 |
| | Kamba-1 | 2014 | BG Tz | Haijaendelezwa | 1.03 |
| **JUMLA YA KIASI CHA GESI ASILIA KILICHOGUNDULIWA BAHARINI** | | | | | **47.13** |
| **JUMLA KUU (TCF)** | | | | | **57.25** |

*Chanzo: TPDC - Aprili, 2016*

***Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Kiasi cha Gesi Asilia Kilichogunduliwa Nchi Kavu na Baharini***




*Chanzo: TPDC - Aprili, 2016*


## B. SEKTA YA MADINI

***Kielelezo Na. 6: Kiasi cha Dhahabu Kilichozalishwa na Kuuzwa na Migodi Mikubwa ya Dhahabu (2006 – 2015)***





*Chanzo: TMAA - Aprili, 2016*

***Kielelezo Na. 7: Thamani ya Madini Yaliyozalishwa na Kuuzwa na Migodi Mikubwa ya Dhahabu (2006 – 2015)***





*Chanzo: TMAA - Aprili, 2016*

***Kielelezo Na. 8: Kiasi cha Mrabaha Kilicholipwa na Migodi Mikubwa ya Dhahabu (2001 – 2015)***




*Chanzo: TMAA - Aprili, 2016*


***Kielelezo Na. 9: Kiasi cha Kodi Mbalimbali kilicholipwa na Kampuni za Uchimbaji Mkubwa wa Madini (2001 - 2015)***




*Chanzo: TMAA - Aprili, 2016*


*Angalizo: Kodi Zinajumuisha - Corporate Tax, Value Added Tax, Pay As You Earn, Skills Development Levy and Withholding Tax.*

***Kielelezo Na. 10: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Dhahabu katika Soko la Dunia (2001 - 2015)***





*Chanzo: LME/LBMA*

***Kielelezo Na. 11: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Madini ya Fedha katika Soko la Dunia (2001 - 2015)***





*Chanzo: LME/LBMA*

***Kielelezo Na. 12: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Madini ya Shaba katika Soko la Dunia (2001 - 2015)***





*Chanzo: LME/LBMA*

***Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Madini ya Urani katika Soko la Dunia (2001 - 2015)***




*Chanzo: NYMEX, CME Group*

***Kielelezo Na. 14: Ununuzi wa Bidhaa na Huduma Uliofanywa na Kampuni za Uchimbaji Mkubwa wa Madini (2006 - 2015)***





*Chanzo: TMAA - Aprili, 2016*

***Kielelezo Na. 15: Takwimu za Ajira za Watanzania na Wageni katika Migodi Mikubwa (2009 - 2015)***

| Jina la Mgodi | Aina ya Ajira | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bulyanhulu | Watanzania | 2,012 | 2,266 | 2,430 | 2,535 | 2,290 | 2,028 | 1,755 |
| | Wageni | 185 | 181 | 195 | 181 | 167 | 138 | 125 |
| | Jumla | 2,197 | 2,447 | 2,625 | 2,716 | 2,457 | 2,166 | 1,880 |
| Buzwagi | Watanzania | 671 | 746 | 875 | 1,064 | 787 | 934 | 899 |
| | Wageni | 49 | 105 | 132 | 104 | 49 | 19 | 10 |
| | Jumla | 720 | 851 | 1,007 | 1,168 | 836 | 953 | 909 |
| Geita | Watanzania | 1,814 | 1,792 | 1,601 | 1,610 | 1,560 | 1,518 | 1,568 |
| | Wageni | 121 | 86 | 82 | 77 | 78 | 67 | 71 |
| | Jumla | 1,935 | 1,878 | 1,683 | 1,687 | 1,638 | 1,585 | 1,639 |
| Golden Pride | Watanzania | 238 | 266 | 297 | 304 | 333 | 0 | 0 |
| | Wageni | 27 | 34 | 37 | 42 | 23 | 0 | 0 |
| | Jumla | 265 | 300 | 334 | 346 | 356 | 0 | 0 |
| New Luika | Watanzania | 0 | 0 | 0 | 0 | 270 | 313 | 421 |
| | Wageni | 0 | 0 | 0 | 0 | 30 | 29 | 36 |
| | Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 300 | 342 | 457 |
| North Mara | Watanzania | 621 | 703 | 876 | 971 | 926 | 976 | 968 |
| | Wageni | 127 | 138 | 157 | 148 | 92 | 68 | 57 |
| | Jumla | 748 | 841 | 1,033 | 1,119 | 1,018 | 1,044 | 1,025 |
| TanzaniteOne | Watanzania | 613 | 648 | 643 | 630 | 645 | 574 | 1,166 |
| | Wageni | 29 | 33 | 32 | 37 | 25 | 16 | 23 |
| | Jumla | 642 | 681 | 675 | 667 | 670 | 590 | 1,189 |
| Williamson | Watanzania | 610 | 584 | 558 | 534 | 551 | 558 | 558 |
| | Wageni | 4 | 8 | 8 | 10 | 10 | 11 | 11 |
| | Jumla | 614 | 592 | 566 | 544 | 561 | 569 | 569 |
| JUMLA KUU | Watanzania | 6,579 | 7,005 | 7,280 | 7,648 | 7,362 | 6,901 | 7,335 |
| | Wageni | 542 | 585 | 643 | 599 | 474 | 348 | 333 |
| | Jumla | 7,121 | 7,590 | 7,923 | 8,247 | 7,836 | 7,249 | 7,668 |

*Chanzo: TMAA - Aprili, 2016*

***Kielelezo Na. 16: Mwenendo wa Uhitimu wa Wanafunzi katika Kozi Mbalimbali katika Chuo cha Madini (MRI) Dodoma (2014/15 vs 2015/16)***




*Chanzo: MRI - Aprili, 2016*